**Nipashe**

Jumatatu Juni 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580252

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710



## 693 wachachamalia malipo kiduchu kupisha mradi gesi

UKURASA 2




UKURASA 11

# Safari ya ushirikiano Chadema, ACT yanukia

**NI** kuelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba...*Endelea ukurasa 2*




Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akimkabidhi wasilisho na muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 20 wa wanahisa wa Benki ya NMB, Mwenyekiti wa Muda wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Margaret Ikongo, baada ya kumaliza mkutano huo uliofanyika kwa njia ya mtandao. Kulia ni Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha, Benedicto Baragomwa.**Habari uk. 5.**
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## BAA LA CORONA



Kutokana na janga la ugonjwa wa corona unaosababishwa na virusi vya Covid-19, watu wengi wanatumia muda wao kukaa ndani ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo. Inashauriwa kufanya mazoezi ya mwili walau dakika tatu mpaka tano ili kunyoosha misuli na kuweka uimara wa mwili, na hii inashauriwa kwa rika zote ili kuweza kupunguza magonjwa nyemelezi. Mazoezi ya kila wakati yanasaidia kuchangamsha akili na mwili pia. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## MAGUFULI ASHUKURU MAOMBEZI YA CORONA

UKURASA 2

### BAADA KUTANGAZA KUSTAAFU

## Lwakatare: Kero hizi ziliniingiza siasa, yaliyonikuta huko ni haya

**SAA 24** aliusamehe uofisa, mishahara 3

UKURASA 4



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store

**MICHEZO** SVEN: WACHEZAJI SIMBA WANAREJESHA VIWANGO UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Ushirikiano Chadema, ACT wanukia

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), vimeonyesha nia ya kushirikiana katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba mwaka huu.

Tayari ACT-Wazalendo imeitikia wito uliotolewa na Chadema wa kushirikiana katika uchaguzi huo kwa kukiandikia barua ya kuanza rasmi mazungumzo ya ushirikiano huo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema siku moja baada ya Katibu Mkuu wa Chadema kutoa wito huo, alimwandikia barua ya kukubali kuingia katika mazungumzo.

"Tumemsikia Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, akisema milango iko wazi kwa chama chochote kushirikiana nao katika uchaguzi mkuu, siku moja tu baada ya kutoa kauli hiyo, mimi kama Katibu Mkuu wa chama changu, nilimwandikia barua kumweleza jinsi ambavyo tumepokea wito huo kwa mikono miwili na kumwonyesha utayari wa kwenda katika ushirikiano ikiwamo kuanza mchakato wa mazungumzo," alisema Shaibu.

" ACT-Wazalendo tunaamini katika ushirikiano kwa sababu ndiyo silaha pekee ya kuhakikisha kwamba CCM itaondoka madarakani mwaka 2020, tukishikamana kwa pamoja na tukaweka tofauti za kiitikadi pembeni tuna fursa kubwa sana ya kuiondoa madarakani."

Shaibu alisema wanaamini kwamba mazungumzo hayo yatafikia katika hatua nzuri.

"Na jambo kubwa katika mambo ya ushirikiano ni utayari, na kama Chadema wameonyesha hilo na wametangaza kwamba mchakato unaweza kuanza na sisi ACT-Wazalendo... tumeonyesha utayari na tumewajibu kwa barua, hiyo inakupa picha kwamba tunakoenda ni kuzuri," alisema Shaibu.

Alisema chama hicho kina matumaini kwamba katika muda uliopo wa kujiandaa na uchaguzi mkuu, watafanikiwa kutengeneza vuguvugu kubwa.

"ACT-Wazalendo bado tuna matumaini makubwa katika muda uliopo, kutengeneza vuguvugu kubwa (movement) litakalohakikisha tunakwenda kwenye uchaguzi katika mshikamano," alisema Shaibu.

Pia alisema kwamba wanahitaji mshikamano huo kwa sasa ili kuwa na nguvu zaidi ya kuwaletea Watanzania maendeleo.

Akizungumzia ratiba ya chama hicho katika kuelekea uchaguzi huo mkuu, Shaibu alisema katikati ya mwezi huu wanatarajia kuzindua rasmi uchukuaji na urudishaji wa fomu za wagombea katika nafasi mbalimbali.

Alisema tayari zaidi ya wanachama 200 wametangaza nia ya kugombea nafasi ya ubunge kupitia chama hicho.

Wiki iliyopita Chadema kilitoa wito kwa vyama vya siasa vyenye nia ya kushirikiana nacho, kupeleka maombi ya kuingia katika mazungumzo rasmi ya ushirikiano huo, kuelekea katika uchaguzi mkuu ujao.

Chama hicho kilitoa wito wa ushirikiano huo katika ngazi zote kuanzia nafasi ya udiwani, ubunge na urais.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Nyakitonto ambao ni wakulima waliolima katika Msitu wa Hifadhi ya Makere Kusini, uliopo Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma, ametoa muda wa mwezi mmoja kuvuna na kuondoa mazao yao na baada ya hapo watakaobainika kuendelea kulima watachukuliwa hatua kali za kisheria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia fidia ndogo mradi wa gesi

**Na Mwandishi Wetu, LINDI**

WANANCHI wa Kata ya Mbanja mkoani Lindi, eneo unakojengwa mradi mkubwa wa kufua gesi (LNG), wameeleza kutoridhishwa na viwango vya fedha walizopewa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kama fidia ya kuhama makazi yao, ili kupisha utekelezaji wa mradi huo.

Mei mwaka huu, TPDC kwa kushirikiana na mashirika mengine ya kimataifa, ilitoa fidia kwa wananchi 693 waliotakiwa kupisha mradi huo, takribani Sh. bilioni 5.2 zilitengwa kwa ajili ya kufanikisha fidia kwa wananchi hao kwenye eneo la mradi lenye ukubwa wa hekta 2,071.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, kiwango cha chini cha fidia kilicholipwa kwa mtu mmoja ni Sh. 400,000 na cha juu Sh. milioni 70.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi hao wamejitokeza na kudai kutoridhishwa na kiasi cha fedha walizopewa, na kuongeza kwamba wakati TPDC ilipofanya tathmini ya ardhi na mali za zao mwaka 2014, iliwaahidi kuwalipa wananchi hao fedha ambazo zingewawezesha kuondokana na umaskini.

"Mwaka 2014, walikuja watu kufanya tathmini kuhusu mpango wa gesi. Maelekezo waliyokuwa wanatupa ni kwamba kutokana na uzoefu wao wa kuwaondoa watu kupisha utekelezaji wa miradi mikubwa kama huu, basi tutanufaika kwa sababu watatulipa vizuri na kutuandalia mazingira mazuri ya makazi mapya.

"Lakini, ilipofika hatua ya malipo, hali imekuwa tofauti na matarajio ya wananchi wengi, kwani waliohamishwa hawawezi kujenga kwa kipato walichokipata na walionyang'anywa mashamba, sidhani kama wanaweza kununua mashamba mengine," alisema Mussa Mwaya, mkazi wa Kijiji cha Likong'o.

Wananchi hao pia wametoa malalamiko dhidi ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na TPDC kwa kuchelewesha malipo ya fidia zao kwa zaidi ya miaka mitano na pia kwa kushindwa kuwalipa baadhi ya wananchi wa kata hiyo hususani kutoka vijiji vya Likong'o na Mtomkavu ambavyo maeneo yake yalishafanyiwa tathmini tangu mwaka 2014, lakini hawajalipwa fidia zao kwa kile walichoelezwa kwamba maeneo yao hayatotumika tena kwa ajili ya mradi huo mkubwa wa gesi.

"Tathmini ilivyofanyika na jinsi walivyokuja na malipo, kwa kweli sisi tumeridhika, lakini kwa upande mwingine hatujaridhika. Walifanya tathmini mpaka majumba yetu, tukashindwa kuyaendeleza kwa sababu tulifahamu tutahama siku siyo nyingi. Kitu cha kushangaza hivi karibuni tuliambiwa hatutohama.

"Ninaiomba serikali ituangalie kwa jicho la huruma kwani tumeshaathirika, majumba yetu mabovu. Ni zaidi ya miaka sita tangu walipofanya tathmini," alililalamika Masoud Masoud, mkazi wa Kijiji cha Likong'o.

Alipoulizwa kuhusu suala hilo, Meneja Mradi wa Gesi, Fedister Agrey, alisema: "Siyo kweli kwamba elimu haikutolewa kwa waathirika wa mradi. TPDC ikisaidiana na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, iliendesha zoezi la utoaji elimu kwa umma wakati wa tathmini na pia kabla ya malipo ya fidia hayajafanyika. Elimu ilihusisha masuala ya haki za binadamu, vigezo na masharti ya fidia na vitu vingine."

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Jomaary Satura, alibainisha kwamba serikali tayari imeshakamilisha malipo ya riba kwa waathirika wa mradi huo kwa kuzingatia vifungu vya Sera ya Ardhi (1995), Sheria ya Ardhi (1999), Sheria ya Ardhi ya Kijiji (1999) zinazoelekeza fidia kulipwa ndani ya miezi sita baada ya tathmini kufanyika, kinyume cha hapo waathirika walipwe riba kulingana na kipindi ambacho fidia haijalipwa.

"Malipo ya fidia kwa waathirika wa mradi yamechelewa kwa miaka mitano, lakini kwa sasa tumeshalipa riba ya miaka mitatu kwanza na zaidi ya Sh. milioni 800 zitatumika kukamilisha malipo ya riba ya miaka miwili iliyobakia," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mtomkavu, Abdlahman Jadu, aliiomba serikali kupima ardhi na ugawaji wa hati kwa wakazi wa kijiji chake ambao maeneo yao yako jirani na eneo la mradi, ili kuwahakikishia wananchi hao umiliki wa ardhi wanayoishi kisheria na kufaidika na ardhi yao itakapofikia hatua ya kuondolewa kupisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na uwekezaji.

"Zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi lilifanyika kwa mafanikio makubwa, lakini malalamiko yamejitokeza kutoka kwa baadhi ya wananchi waliolipwa fidia ndogo kutokana na hatua ya TPDC kuondoa suala la thamani ya ardhi kwenye malipo ya fidia kwa maelezo kwamba wananchi walikuwa wamevamia eneo hilo ambalo lilikuwa ni shamba la mkonge na baadaye kubinafsishwa na kuchukuliwa na serikali," alisema.

Alisema faida zingine ambazo baadhi ya wananchi waliondolewa eneo la mradi, ni pamoja na kupatiwa viwanja vilivyopimwa kwa ajili ya kuanzisha makazi mapya na kuuziwa mashamba kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Mei mwaka jana, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema utekelezaji wa mradi huo utaanza rasmi mwaka 2022 na kumalizika mwaka 2028.

# JPM ashukuru viongozi dini maombezi corona

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amewashuruku viongozi wa dini na Watanzania kwa kuitikia wito wa maombezi ya kupusha janga la ugonjwa wa corona.

Alitoa shukurani hizo jana, alipokaribishwa kuwasalimia waumini wa Kanisa la Katoliki, Parokia ya Bikira Maria Imakulata, Chamwino mkoani Dodoma, baada ya kuhudhuria Misa Takatifu ya Sikukuu ya Utatu Mtakatifu iliyoongozwa na Paroko wa Parokia hiyo, Padri Paulo Mapalala.

Rais Magufuli alisema Mungu amejibu maombi ya Watanzania ambao wamesali, kufanya toba pamoja na kufunga, na matokeo yake ni kuwa maambukizo ya virusi vya corona yamepungua.

Rais Magufuli alisema wananchi wanaendelea na maisha yao, huku wakichapa kazi za uzalishaji mali, tofauti na ilivyodhaniwa kuwa ugonjwa huo ungesababisha madhara makubwa.

Aidha, Rais Magufuli alitoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuwa makini dhidi ya mbinu zozote zinazoweza kufanywa kuwaambukiza ugonjwa huo ama magonjwa mengine, huku wakimshukuru na kumtumaini Mungu aliye muweza wa yote.

Akiwa kanisani hapo, Rais Magufuli aliendesha harambee ya kuchangia upanuzi wa kanisa hilo na kufanikiwa kuchangisha Sh. milioni 17.229, kati ya fedha hizo Sh. milioni 10 akizitoa yeye.

Pia katika harambee hiyo ilipatikana mifuko 76 ya saruji, na kuagiza upanuzi wa kanisa hilo uanze leo.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Taasisi ya Al Hekma, Shekhe Nurdin Kishik (wa pili kulia), na Katibu wa Taasisi ya Task Forc, Ally Abdallah (katikati), akikabidhi msaada wa mbegu ya mahindi na vyakula kwa mkazi wa Mtunda, Kata ya Mtunda Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani, Asia Amiri, uliotolewa na Taasisi za Kiislam kutoka kwa Watanzania wenye asili ya Yemen, kwa niaba ya wakazi wa kata hiyo, waliokumbwa na mafuriko yaliyoharibu makazi yao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TBA yasimamishwa ujenzi halmashauri

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameusimamisha Wakala wa Majengo (TBA) kuendelea na ujenzi jengo la Halmashauri ya Madaba wilayani Songea.

Mndeme alitangaza kuchukua uamuzi huo baada ya TBA kushindwa kukamilisha mradi huo kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, licha ya serikali kutoa zaidi ya Sh. bilioni 2.2 za utekelezaji wake.

"Mimi silei wabadhirifu na wahujumu, kuanzia leo (jana) hatuwaongezei tena muda, kuanzia sasa TBA, msimame ujenzi wa jengo hili na ujenzi wake utaendelea kwa kutumia 'force account', pia ninaagiza kuanzia leo Takukuru waanze kuchunguza mradi huu," aliagiza.

Mndeme aliagiza Takukuru kuchunguza sababu za mradi huo kusuasua na kuchukua muda mrefu na kwamba iwapo kuna mtu yeyote amefanya hujuma dhidi ya mradi huo, achukuliwe hatua haraka.

Aliwataka TBA wanapoomba kazi, kuhakikisha wanakamilisha kazi kwa wakati, akieleza kuwa licha ya kuongezewa muda wa mkataba mara mbili, bado wameshindwa kukamilisha mradi huo.

Aliwatahadharisha TBA wasihangaike kuomba kazi za ujenzi ndani ya Mkoa wa Ruvuma kwa sababu miradi yote waliokuwa wanatekeleza ndani ya Mkoa wa Ruvuma wameshindwa kuikamilisha.

Mndeme alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Songea, kuhakikisha anasimamia mradi huo wakati, ambao sasa unakamilishwa kwa 'force account' kwa wakati na viwango na kwamba serikali hivi sasa inatekeleza kwa wakati na viwango miradi mingi kwa 'force account'.

Mhandisi Mshauri wa mradi huo kutoka Kampuni ya BICO, Ahmed Nyange, alisema mradi huo ambao umefikia asilimia 84, ulitarajiwa kukamilika Januari 20 mwaka huu, lakini mkandarasi aliongezwa miezi minne hadi Mei 31 mwaka na ameshinda kukamilisha mradi.

Nyange alisema hadi sasa mkandarasi ameshalipwa zaidi ya Sh. bilioni moja, sawa na asilimia 61 ya gharama yote ya mradi na kwamba mkandarasi ameshindwa kukamilisha mradi kwa wakati, hivyo BICO inaunga mkono kukamilisha mradi kwa 'force account'.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba, Shafii Mpenda, alisema TBA imekuwa na dosari nyingi ambazo zimekuwa zinajitokeza mara kwa mara na kusababisha mradi kushindwa kukamilika kwa wakati.

"Ninasikitika kusema kwamba imebidi tufikie hapa tulipofika ili kunusuru mradi na fedha za umma, tusitishe mkataba na TBA na tuombe ridhaa kutoka kwa Katibu Mkuu wa Tamisemi, ili aridhie kukamilisha kazi zilizobaki kwa kutumia 'force account'," alisema.

Awali, Mwakilishi wa TBA, Elias Tillya, alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kuwa walianza vizuri utekelezaji wa mradi huo na walitarajia Juni mwaka huu kukabidhi jengo hilo.

Hata hivyo, alisema kuwa mwishoni mwa Mei mwaka huu, TBA ilipata vikwazo kwenye akaunti zake katika mikoa yote nchini, hali ambayo ilisababisha kushindwa kutoka fedha baada ya akaunti zake zote kuzuiwa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
02 – 06 - 2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **09 – 06 – 2020** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam kuelekea Mlandizi,** gari hizo zenye namba za usajili:

   **T 133 CCP / T 887 DJB T 135 CCP /T 837 DJB T 914 DSD /T 387 DHQ T 868 DDL /T 390 DHQ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **25** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.2** |

3. Njia itakayotumika: **Morogoro Road,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# Wauawa na fisi wakisaka maji

**Na Marco Maduhu, KAHAMA**

WANAWAKE wanaoishi Kata ya Ngongwa wilayani Kahama, wamedaiwa kuwa hatarini kutokana na kuwapo na tishio la fisi pindi wanapofuata maji nyakati za usiku.

Imeelezwa kuwa tayari wanyama hao wameshasababisha vifo kwa wanawake wawili katika eneo hilo.

Diwani wa Ngogwa, Kamuli Mayunga, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama wilayani Kahama, iliyokuwa na lengo la kukagua mradi wa majisafi na salama ulioko katika kata hiyo.

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka za Maji za Shuwasa, Kuwasa na Ruwasa, una thamani ya Sh. bilioni 2.4.

Mayunga alisema wanawake wa Ngongwa maisha yao yamekuwa hatarini kwa miaka mingi kutokana na uwapo na adha ya maji na hulazimika kuamka majira ya usiku ili kufuata maji umbali mrefu, ambako njiani hukutana na fisi na kuanza kuwakimbiza.

Alisema wanyama hao wamekuwa wakiwajeruhiwa wananchi huku wawili wakiuawa.

"Maeneo yetu haya ya Ngongwa kuna fisi wengi sana kwa sababu ya uwapo na milima, na wamekuwa tishio kwa wanawake, wahatarisha maisha yao wanapokuwa wakifuata maji nyakati za usiku.

"Miaka miwili iliyopita, tulipoteza wanawake wawili sababu ya kushambuliwa na fisi hawa," Mayunga alisema.

Baadhi ya wanawake wa Ngongwa akiwamo Celina Paulo, walikiri fisi hao kuwa tishio kwa maisha yao, huku wakiomba mradi huo wa maji ukamilike kwa wakati ili kuwaondolea adha hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shuwasa), Flaviana Kifizi, alisema mradi huo wa maji umekamilika kwa asilimia 95 na utaisha Agosti mwaka huu ukigharimu Sh. bilioni 2.4 na utanufaisha zaidi ya wakazi 1,000.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alipongeza utekelezwaji wa mradi huo wa majisafi na salama, huku akiwataka wananchi waitunze miondombinu yake ili idumu kwa muda mrefu.

**"Maeneo yetu haya ya Ngongwa kuna fisi wengi sana kwa sababu ya uwapo na milima, na wamekuwa tishio kwa wanawake, wahatarisha maisha yao wanapokuwa wakifuata maji nyakati za usiku.**


**Air Tanzania**
*The Wings of Kilimanjaro*

**TRAINING INSTITUTE**
**KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)**

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Institute ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 13/07/2020. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/06/2020.
Sifa za mwombaji.

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini ya kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae -CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Institute**
**S.L.P 543**
**Dar es salaam**
**Barua pepe: training@airtanzania.co.tz**
**Simu ya mkononi: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING INSTITUTE.**



MAHOJIANO MAALUM

## BAADA KUTANGAZA KUSTAAFU

# Lwakatare: Kilichoniingiza siasa kero hizi, niliyoyakuta haya hapa

## Saa 24 aliusamehe uofisa, mishahara 3



**Na Sanula Athanas, DODOMA**

SHAUKU iliyopitiliza kudai haki ndiyo ilimfanya Wilfred Lwakatare (pichani), Mbunge wa Bukoba Mjini, aitose ajira yake ya ofisa utumishi na utawala na kuilipa serikali mishahara mitatu ndani ya saa 24 ili ajiunge na siasa, Nipashe imeelezwa.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe wiki iliyopita, Lwakatare (56), alisema ni uamuzi aliouchukua mwaka 1998, kipindi hicho akiitumikia Manispaa ya Bukoba baada ya kubaini anashindwa kuwa na uamuzi mkubwa dhidi ya mlolongo wa uonevu, madai yalipowasilishwa mezani kwake.

"Ni kweli mimi siasa niliziingia mwaka 1991 nikiwa mtumishi wa Halmashauri ya Mji Bukoba (wakati huo na kwa sasa manispaa)... Nilivyoingia kazini tangu mwanzo 1989, nilipenda utetezi wa haki kwa watendaji, kutetea na kuilinda haki za watumishi kazini.

"Uvunjifu na unyimaji haki watumishi, ni jambo lililokuwa likinikera wazi na mimi kulisemea. Japo nilikuwa ofisa utumishi, nafasi yangu haikuwa ya matawi ya juu yenye nguvu ya kuamua na kutenda.

"Hivyo, niliishia kwenye 'frustrations', jambo lililonipelekea mwaka 1998 kumwandikia mwajiri 'notice' ya saa 24 ya kuacha kazi na hivyo kumlipa pesa 'cash' (taslimu) mishahara yangu ya miezi mitatu kwa mujibu wa sheria za kazi.

Na hapo ndiyo ukawa mwanzo wa mimi kuingia kwenye siasa moja kwa moja na mwaka 2000 kufanikiwa kugombea ubunge Jimbo la Bukoba Mjini na kushinda kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF)," alisema.

Katika mazungumzo hayo ya faragha na Nipashe, Lwakatare pia aligusia hatua zilizochukuliwa dhidi yake na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kilichomsukuma kuamua kutowania tena ubunge. Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo ya Nipashe na Mkurugenzi huyo wa zamani wa Idara ya Ulinzi na Usalama ya Chadema:

---

***SWALI: Ulikuwa ofisa wa Halmashauri ya Bukoba. Nini hasa kilikuingiza katika siasa za ubunge, tena upinzani?***

**LWAKATARE:** "Ni kweli mimi siasa niliziingia mwaka 1991 nikiwa mtumishi wa Halmashauri ya Mji Bukoba (wakati huo na kwa sasa manispaa) na mwaka mmoja kabla ya mfumo wa vyama vingi kuruhusiwa kisheria.

Historia yangu shuleni kuanzia elimu ya msingi, secondarI 'O' na 'A' Level na kisha JKT mwaka mmoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 1985-1988, kwa wote niliobahatika kuwa nao, ni mashahidi wangu kuwa mimi ni mtu mwenye hulka ya kupenda kuhoji 'logically' mambo yoyote yanayojitokeza ndani ya taasisi husika yenye kuzua utata au kuibua hoja shindanishi.

Ni mtu niliyependa mijadala na nilisoma na kuyapenda masomo ya 'literature' (fasihi), fasihi simulizi na andishi. Ukweli nimekuwa mwathirika mkubwa wa 'carrier' yangu kimasomo.

Nilivyoingia kazini tangu mwanzo 1989, nilipenda utetezi wa haki kwa watendaji, kutetea na kulinda haki za watumishi kazini, huku nikiwa Ofisa Utumishi na Utawala.

Hali hiyo inipelekea kutunukiwa ufanyakazi bora mara mbili ndani ya kipindi changu cha miaka 13 ya utumishi serikalini na katika vituo mbalimbali. Hivyo, uvunjifu na unyimaji haki watumishi, ni jambo lililokuwa likinikera wazi na mimi kulisemea.

Japo nilikuwa Ofisa Utumishi, nafasi yangu haikuwa ya matawi ya juu yenye nguvu ya kuamua na kutenda. Hivyo niliishia kwenye 'frustrations', jambo lililonipelekea mwaka 1998 kumwandikia mwajiri 'notice' ya saa 24 ya kuacha kazi na hivyo kumlipa pesa 'cash' mwajiri mishahara yangu ya miezi mitatu kwa mujibu wa sheria za kazi.

Na hapo ndiyo ukawa mwanzo wa mimi kuingia kwenye siasa moja kwa moja na mwaka 2000 kufanikiwa kugombea ubunge Jimbo la Bukoba Mjini na kushinda kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF).

***SWALI: Ulionaje joto la siasa na nini siri ya ushindi wako?***

**LWAKATARE:** Kila uchaguzi una joto lake kufuatana na aina ya uchaguzi, awamu ya utawala na namna 'inavyo-respond' na sheria, kanuni na taratibu zinazokuwa zimewekwa katika kipindi husika.

Mimi nilianza kushiriki uchaguzi kwa mara ya kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1994 nilipoamua kugombea uenyekiti wa mtaa -- Mtaa wa Omukituli, kata yangu ya nyumbani Kibeta, Bukoba mjini kwa tiketi ya CUF nikiwa mtumishi wa serikali.

Uchaguzi huo ulikuwa na vikwazo vikubwa ukichukulia maanani kuwa ulikuwa uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi serikali za mitaa baada ya sheria ya vyama vingi kupitishwa mwaka 1992.

Katika uchaguzi huo, uongozi wa mkoa na wilaya wa chama na serikali, ulilazimika kuja kumfanyia kampeni mgombea wa CCM katika mtaa wetu nilikogombea mimi.

Ninamshukuru Mungu na wakazi wenzangu wa Mtaa wa Omukituli walinichagua kwa kura nyingi mno. Washindani wangu waliondoka kwa aibu sana. Kiukweli iliwauma sana utafikiri ulikuwa uchaguzi wa kumpata mbunge.

Uzuri waliridhika na matokeo, wakayakubali na kuondoka kwenda kuugulia maumivu bila kuleta vurugu au kutumia nguvu. Na mimi nikaendelea na kazi bila kubughudhiwa.

Ukilinganisha hali hiyo na hali tunayoishuhudia hivi vipindi tunavyopita, ni mambo tofauti ya ajabu. Nikipata fursa na nafasi huko mbele, nitakuja siku moja kuwaelezeni na kuwapa 'facts' za uchaguzi uliofuata kwa miaka yote ya uchaguzi, kwani nilishiriki kwa vitendo, nikashinda na kushindwa.

***USIKOSE KESHO KUFUATILIA MFULULIZO WA MAZUNGUZO HAYA**

# Wiki mbili maonyesho ya Sabasaba kidigitali zaja

**Na Elizabeth Zaya**

MAONYESHO ya 44 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), yanatarajia kuanza Julai Mosi hadi 13 mwaka huu, katika Uwanya wa Maonyesho wa Julius Nyerere.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, uratibu wa maonyesho hayo unazingatia kanuni za afya kwa lengo la kuchukua hatua za kujikinga na maambukizo ya corona.

Ilielezwa kuwa mikutano ya ana kwa ana ya wafanyabiashara (B2B) mwaka huu itaandaliwa na kuratibiwa kwa njia ya mtandao.

Pia, watembeleaji watakuwa wananunua tiketi kupitia simu za mikononi, huku watembeleaji wengine wa ndani na nje ya nchi wakipewa fursa kufuatilia maonyesho hayo kupitia mitandao itakayokuwa inarusha moja kwa moja.

"Uratibu wa maonyesho unazingatia kanuni za afya kwa lengo la kuhakikisha kuwa uwanja wa maonyesho unakuwa salama kwa waonyeshaji na watembeaji kwa kuchukua hatua stahiki za kujikinga na maambukizo ya Covid-19," alisema Bashungwa katika taarifa yake hiyo.

"Ili kurahisisha, watembeleaji wa maonyesho watapata fursa ya kununua tiketi kupitia simu za mikononi, watembeleaji kutoka ndani na nje ya nchi watapata fursa ya kutembelea maonyesho hayo kupitia mitandao na kutakuwa banda maalum la kutangaza bidhaa za kilimo yakiwamo mazao ya kimkakati," aliongeza.

Waziri Bashungwa alitoa wito kwa wafanyabiashara, wamiliki wa viwanda vyote nchini, wakulima, taasisi za umma, halmashauri za wilaya na taasisi binafsi, kushiriki katika maonyesho hayo ili kuongeza wigo wa masoko ya kilimo, viwanda, mifugo, uvuvi na madini.



Wakazi wa Kibiti mkoani Pwani wakijaribu kulinasua gari lililonasa katika tope juzi, kutokana na barabara kuharibika. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanahisa wa NMB kulipwa gawio bil. 48/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB Plc. (NMB) imepitisha kulipa gawio la Sh. 96 kwa kila hisa kwa wanahisa wake.

Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Benki ya NMB umepitisha azimio la kulipa gawio la shilingi bilioni 48 kwa wanahisa, kiasi kilichopendekezwa na benki hiyo wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka, uliofanyika jana kwa njia ya mtandao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema ongezeko hili la gawio lina akisi mafanikio ya kibiashara ya mwaka 2019 na hali nzuri ya ukwasi na mtaji wa benki ya NMB.

Alisema gawio lililopitishwa la shilingi bilioni 48 au shilingi 96 kwa hisa ni ongezeko la asilimia 45 ikilinganishwa na gawio la shilingi bilioni 33 au shilingi 66 kwa hisa lililolipwa mwaka 2018, sawa sawa na sera ya benki ya kulipa theluthi moja (asilimia 33.3) ya faida baada ya kodi kama gawio. Nia ni kuendelea kukuza kiwango cha gawio kwa wanahisa mwaka hadi mwaka.

Kwa mujibu wa Zaipuna, kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2019, Benki ilipata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 142 ikiwa ni ongezeko la asilimia 46 kutoka faida ya shilingi bilioni 98 iliyopatikana mwaka 2018.

Alifafanua kuwa kuongezeka kwa faida ya benki kulitokana na kuongezeka kwa mapato ya uendeshaji, kupungua kwa tengo la mikopo chechefu na juhudi za kupunguza matumizi ya kiuendeshaji yaliyopelekea benki kumaliza mwaka 2019 bila ongezeko la gharama za uendeshaji.

Kutokana na faida kuongezeka, Bodi na Uongozi wa Benki ya NMB umeridhishwa na matokeo chanya yaliyotokana na mapinduzi ya kiteknolojia na kuimarishwa kwa huduma za kibenki katika kipindi cha mwaka 2019. Mapinduzi hayo ni pamoja na uzinduzi wa huduma za kibenki kwa njia za kidigitali kama NMB Mkononi na kwa njia ya mtandao wa intaneti maarufu kama "NMB Direct" huku yakichagizwa na huduma mbadala za kibenki kupitia NMB Wakala.

Uimara wa NMB kama Taasisi ya Fedha ulipelekea Moody kuipa alama ya B1 ambayo imethibitisha kuaminika kwa Benki ya NMB katika soko la mitaji nchini na kimataifa.

Mwenyekiti wa Muda wa Bodi ya Wakurugenzi, Margaret Ikongo, alibainisha kuwa bodi inataka kuongeza zaidi pato la wanahisa sambamba na kuongeza uwekezajib.

"Kwa miaka kadhaa sasa NMB imeendelea kuwa imara kwenye sekta ya fedha hasa kimtaji na dhamira yetu ni kuendelea kuimarika zaidi. Ili kufikia mafanikio haya, tunapaswa kuhakikisha tunafanya maamuzi sahihi katika udhibiti wa mabadiliko yoyote ya kimtaji," alisema Ikongo.

"NMB imejipambanua katika kuendelea kuchangia maendeleo ya uchumi Tanzania kupitia kupanua wigo wa mikopo ya watu binafsi, mikopo ya biashara, kilimo, huduma za bima na mikopo ya ujenzi," alisema Zaipuna.

Alisema, matokeo mazuri ya mwaka 2019 yanaonyesha juhudi za uongozi wa benki kuboresha mkakati wake kibiashara unaoweka kipaumbele maeneo matatu yaani, kuongeza amana, kuongeza mapato na ufanisi wa kiutendaji.

# Wakulima wasaidiwa mapambano corona

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAKULIMA na wadau wa kilimo wameendelea kuwezesha katika vita dhidi ya maambukizo ya corona, kwa kupewa vifaa vya kujikinga.

Uwezeshaji huo umefanywa na kampuni ya utengezezaji na usambazaji wa mbolea Yara Tanzania kwa kugawa vifaa saidizi kwa mawakala wake na wakulima wa Kanda ya Kaskazini, ili wajikinge huku wakiendelea na shughuli zao za kilimo.

Tukio hilo lilishuhudiwa na Katibu Tawala Msaidizi-Utawala, David Lyamongi, ambaye aliongozana na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Wedson Sichalwe na wataalamu wanaohusika na mapambano dhidi ya Covid-19.

Lyamongi aliishukuru Yara kwa kuwa mstari wa mbele kwa kuwajali wakulima na mawakala ambao ndio watumiaji wa bidhaa ya mbolea inayotengenezwa na Yara, huku akiwataka mawakala hao waliowakilisha wakulima kuhakikisha vifaa hivyo vinawafikia walengwa ili waweze kujikinga na ugonjwa huo.

"YARA wameamua kumlinda mkulima ikizingatiwa kuwa Tanzania inategemewa sana na nchi jirani katika uzalishaji wa chakula," alisema na kuwaomba waulima wote wazingatie maelekezo yote yaliyotolewa na Wizara ya Afya ikiwamo kunawa mikono na maji tiririka na sabuni, kutumia vitakatishi na kuepuka mikusanyiko wakati wa shughuli za kilimo.

Alisema Yara ni mdau mkubwa kwenye sekta ya kilimo na imekuwa ikishirikiana na serikali kwa karibu katika jitihada mbalimbali za kuboresha kilimo nchini.

Meneja Biashara wa Yara Kanda ya Kaskazini, Phillipo Mwakipesile, alisema vifaa saidizi vilivyotolewa ni vitakatishi, ndoo za kunawia na sabuni, huku akibainisha kuwa kampuni hiyo imetumia Sh. milioni 82 kwa vifaa hivyo katika kanda tatu ambazo ni Kaskazini, Kusini na Magharibi.

Alisema wametoa msaada huo kwa wadau hao muhimu ili kuiunga serikali mkono katika vita dhidi ya homa hii iliyotikisa dunia nzima na kusababisha maafa makubwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi nyingi kwani shughli nyingi za uzalishaji zimesimama.

Alitoa wito kwa wanufaika kuhakikisha wanatumia vifaa hivyo ipasavyo na kuomba wadau wengine pia waunge mkono jitihada hizi ili iwe vita ya pamoja dhidi ya Covid-19.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF imulike mechi hizi Ligi Kuu ikirejea

HATIMAYE Ligi Kuu Bara inarejea rasmi Jumamosi wiki hii kwa Yanga kucheza mechi yake ya kiporo cha raundi ya pili dhidi ya 17 dhidi ya Mwadui FC katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Kambarage mkoani Shinyanga.

Ligi hiyo inarejea baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu, Covid-19, ambao hadi kufikia jana mchana duniani kote ulishasababisha jumla ya vifo 402,438 miongoni mwao wakiwamo Watanzania 21.

Katika vifo hivyo vilivyotokana na ugonjwa huo ambao hadi sasa haujapata tiba wala chanjo, ni kutoka katika wagonjwa 6,993,767 ambao walithibitika kupata maambukizo ya virusi vya corona huku 3,419,952 wakipona. Hata hivyo, kurejea kwa ligi hiyo nchini, kumetokana na serikali kujiridhisha na kasi ya kupona kwa wagonjwa na kupungua kwa asilimia kubwa ya maambukizo, jambo ambalo imeruhusu irejee huku tahadhari zote kama inavyoagizwa na Wizara ya Afya zikichukuliwa.

Tayari Shirikisho la Soka la Tanzania (TFF) pamoja na Bodi ya Ligi (TPLB), wameshapewa taratibu zote zinazostahili kufuatwa kutoka wizara ya michezo na ile ya afya, hivyo kutangaza ratiba ya ligi hiyo ambayo itaanza kwa timu zenye viporo kuvimalizia kwanza ili zote kufikia raundi ya 29 zilipo nyingine.

Na wakati ligi hiyo ikirejea ili kuhitimisha msimu huu wa 2019/20, tunaikumbusha TFF na TPLB kuongeza umakini hususan kwa mechi zinazochezwa nje ya Dar es Salaam ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kila msimu kutokana na ujanja unjanja mwingine nje na ndani ya uwanja ikiwamo shutuma za upangaji matokeo.

Tunatambua kwa miaka mingi Ligi Kuu na hususan mechi ambazo hazirushwi mubashara kupitia televisheni, kumekuwa na michezo michafu mingi ambayo imekuwa ikifanyika ama kwa timu zinazosaka nafasi ya kutwaa ubingwa au zinazopigania kujinusuru kushuka daraja dhidi ya zile zisizokuwa na "chakupoteza" (zenye uhakika wa kubaki Ligi Kuu huku zikiwa hazina nafasi ya kutwaa ubingwa).

Kutokana na klabu ya Simba kuwa katika nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa, tunatambua mchezo mchafu utakuwa ukichezwa na zisizokuwa na chakupoteza dhidi ya zile zinazohaha kubaki Ligi Kuu msimu ujao, hivyo TFF na TPLB, wanapaswa kuzimulika zaidi ili kutoruhusu mwanya kwa timu yoyote kubebwa.

Tunataka kuona kila timu ikibaki ama kushuka kutokana na uwezo wake na si kutumia mbinu mbadala za nje ya uwanja ili kubaki Ligi Kuu msimu ujao, na kama TFF na TPLB watalitekeleza hilo, ni wazi ligi yetu itazidi kuwa ya ushindani zaidi na kuongeza msisimko ndani na nje ya nchi.


Hilo likitokea pia ni wazi udhamini utaongezeka kwenye ligi na hata kwa klabu shiriki, jambo ambalo litaifanya Ligi Kuu Bara kuwa bora na kuimarika kwa maslahi ya wachezaji, hivyo ushindani kuongezeka zaidi.vSi hilo tu, ligi bora pia ni chanzo cha kupata wawakilishi bora wa michuano ya kimataifa; Ligi ya Mabingwa na hata Kombe la Shirikisho Afrika licha ya kwamba mwakilishi wa shirikisho huwa ni bingwa wa Kombe la FA. Aidha, kuimarika kwa ligi pia ni chanzo cha nchi kuwa na timu bora ya taifa hususan kwa Tanzania ambayo wachezaji wake wengi hucheza soka la ndani.

Pamoja na kuitaka TFF na TPLB kumulika Ligi Kuu, lakini inapaswa kutoisahau Ligi Daraja la Kwanza ambapo timu mbili zitakazoongoza kutoka katika Kundi A na B, zitapanda Ligi Kuu moja kwa moja, huku zile zitakazoshika nafasi ya pili zikicheza mechi za mchujo na mbili kutoka Ligi Kuu na washindi kuwa miongoni mwa 18 zitakazoshiriki Ligi Kuu msimu ujao. Nipashe linafahamu Ligi Daraja la Kwanza ndipo kulipo na uozo mkubwa wa shutuma za upangaji matokeo, hivyo haitakuwa vema kwa TFF na TPLB kuelekeza nguvu kwa kutafuta ubora Ligi Kuu na kuacha timu zisizostahili zipande kutoka Ligi Daraja la Kwanza.

Tunaamini TFF na TPLB watakuwa makini katika hatua hii ya lala salama ili kuwafanya wadau na mashabiki wa soka ambao ni mchezo unaoongoza kwa kupendwa zaidi duniani, msimu ujao kushuhudia Ligi

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Serikali sikivu imewasikia, sasa visizingizio visiwepo Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

WIKI kadhaa zilizopita klabu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara, hasa zile zilizoonekana zipo chini ya msimamo zilikuwa zikipinga ligi hiyo kuchezwa kwa vituo.

Ikumbukwe baada ya serikali kuruhusu michezo kurejea, awali ilitangaza Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara kuchezwa kwa vituo.

Na Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza kupigwa Jumamosi ilitakiwa kuchezwa Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar ers Salaam, Uhuru na Azam Complex na Ligi Daraja la Kwanza na la Pili ilipangwa Kituo cha Mwanza, katika Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana.

Viongozi wa klabu za Ndanda, Mbeya City, Mbao FC, Ruvu Shooting, Singida United na nyingine ambazo ukiangalia kwenye msimamo wa ligi haziko nafasi nzuri, walionekana kupinga mfumo huo, wakitaka urejeshwe ule ule wa zamani wa nyumbani na ugenini.

Nakumbuka wakati huo, serikali ilikuwa bado haijatangaza ruhusa ya mashabiki kuingia uwanjani, lakini bado viongozi hao wakataka timu zao zicheze nyumbani na ugenini, ili zipate faida ya kucheza nyumbani, hata kama uwanja utakuwa ni mtupu.

Nakumbuka msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire alikuja na mahesabu ya kuishi Dar kwa siku 30, matumizi ya hoteli, chakula na usafiri wa ndani.

Katika kukokotoa mahesabu yake, ikaonekana kuwa kuishi Dar itakuwa ghali zaidi tofauti na timu kusafiri kwenda mikoani kucheza mechi zao zilizosalia kwa sababu huko, zitakuwa zikikaa siku moja na kurejea makwao.

Serikali sikivu ikasikia kilio chao. ikaruhusu mechi kuchezwa nyumbani na ugenini, lakini kizuri zaidi ikaruhusu na mashabiki kuingia japo ni lazima tahadhari zote za ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi ya corona, lazima zizingatiwe.

Kwa uzoefu wangu wa masuala ya michezo, nilielewa ni kwa nini viongozi wengi walikuwa wakipinga mechi zilizobaki za Ligi Kuu msimu wa 2019/20 uliosimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19.

Ni kwamba timu nyingi ambazo ziko kwenye ukanda wa hatari, zilikuwa zinaogopa kucheza Dar, badala yake zilikuwa zinataka kucheza nyumbani ili kupata sapoti kwa ajili ya kuhakikisha hazishuki daraja.

Hofu ya kurudi Ligi Daraja la Kwanza ndiyo iliyokuwa ikizikumba timu hizo kiasi cha kutaka ligi iendelee kwa mtindo ule ule, zikitegemea kufanya vema kwenye mechi zao zitakazocheza nyumbani.

Mimi sitaki kujua, ni kitu gani ambacho wanategemea zaidi, au wana uhakika kuwa timu zao zitakuwa zikipata ushindi zinapokuwa nyumbani, lakini tayari zimeshapata faida hiyo.

Kila timu sasa itacheza nyumbani na ugenini. Kila moja inatakiwa kuchanga karata zake vizuri na kushinda mechi, si za nyumbani tu, bali hata ugenini.

Tumeona msimu huu baadhi ya timu zikishinda hata ugenini. Mfano Coastal Union, iliichapa Namungo FC mabao 3-1 Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Naipongeza serikali kwa kurudisha mfumo ule ule kwa sababu baadhi ya timu zingepata visingizio kama zingepoteza mechi zake, au kushuka daraja.

Lakini kwa sasa hakuna visingizio tena. Mtindo ni ule ule, nyumbani na ugenini. Timu inayojiweza ishinde ugenini na nyumbani. Hata zile timu zinazoshinda nyumbani tu, haina tatizo, lakini mwisho wa siku pointi ndizo zitaamua.

Kwa sasa hatuhitaji visingizio tena, timu zitakazobaki zitakuwa zimebaki kwa uwezo wao na zile zitakazoshuka zitashuka kwa sababu hazikuwa na uwezo wa kushindana na si kwa sababu mechi zake zimechezea Dar es Salaam, au nje ya mkoa wao.

# Wataalamu wa afya sasa kufunzwa tiba asili, mbadala

**Na Mary Geofrey**

TANZANIA inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya tiba asili na tiba mbadala kwa wataalamu wa afya, kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii ikiwamo ya umuhimu wa matumizi ya dawa za asili katika kutibu maradhi sugu kama kisukari na shinikizo la damu (PB).

Kampuni ya Kimataifa ya Cornwell Tanzania imeamua kuanzisha chuo hicho nchini, baada ya kubainika kuwapo kwa dawa nyingi za asili zenye uwezo wa kutibu magonjwa yote yaliyoshindika hivyo kupitia chuo hicho watu wataweza kuzifahamu na kujifunza ni kwa namna gani zinafanya kazi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati akitangaza rasmi kuanza kwa chuo hicho, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Elizabeth Lema, alisema chuo hicho kitatumika pia kutoa elimu kwa jamii juu ya virutubishi ambavyo mtu anapaswa kula ili asiweze kupata magonjwa.

"Chuo kitaanza rasmi Julai Mosi mwaka huu, tutakuwa tunatoa kozi fupi na ndefu, mwombaji kwa kozi fupi anatakiwa awe na elimu ya kidato cha nne na mwenye kiwango cha ufaulu wa alama D kwenye masomo ya kemia na baiologia, kwa kozi ndefu mwombaji pia anatakiwa awe amepata alama ya D katika masomo ya Kemia na Baiolojia ni zitakuwa kuanzia miaka miwili," alisema Lema.

Alisema uwapo wa chuo hicho hapa nchini itaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki kufundisha masuala ya tiba mbadala, hivyo anawaomba wale wote wenye nia ya kusoma kujitokeza kwa wingi ili kuweza kupata mafunzo hayo.

"Tunawakaribisha wataalamu wa afya ambao wanapenda kuongeza utaalamu wa tiba mbadala kuweka wigo mpana katika kazi yao, kwa yeyote anayehitaji kusoma afike katika vituo vyetu kupata maelezo," alisema Lema.

Alisema pamoja na kozi hizo watakuwa wakitoa elimu sahihi ya matumizi ya dawa asili na virutubisho kwa yeyote atakayetaka kujua na kutumia yeye na familia yake hasa zile zenye wagonjwa waliokuwa wanatumia dawa kwa muda mrefu.

Alisema kampuni hiyo tayari ina shamba la miti dawa lililopo Pemba Mnazi Kigamboni ambapo ndipo wanavuna na kuitumia kutengeneza baadhi ya dawa zao ikiwamo za virutubisho.

Mkurugenzi mwenza wa kampuni hiyo, Johny Brinkmann, alisema anaona fahari kuanzisha chuo hicho nchini ambacho pamoja na kutoa elimu kitatambulisha dawa za asili na matumizi yake kwa binadamu.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, wakati wa kutoa taarifa ya kupata faida ya kodi ya Sh. bilioni 15.9. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Dk. Edmond Mndolwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aonya ugawaji wa vitambulisho machinga

**Na Welingtone Masele, TABORA**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amewaonya watendaji wa vijiji, kata na maofisa tarafa katika wilaya zote za mkoa huo watakaoshindwa kugawa vitambulisho vya wajasiriamali walivyokabidhiwa na serikali.

Mwanri alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa katika ziara ya kuhamasisha wananchi wa Wilaya za Kaliua, Urambo na Sikonge kuchangamkia vitambulisho hivyo kabla havijaisha, ili viwasaidie pamoja na kuondoa usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza wakati wakiendelea na shughuli za biashara ndogondogo.

Alisema wananchi wa Mkoa wa Tabora wamekuwa na mwitikio mkubwa ambapo mwaka jana mkoa ulikuwa wa kwanza kumaliza zoezi hilo kwa kuuza vitambulisho 65,000 na mwaka huu wamepewa 71,500, ambavyo vimepangwa kuuzwa kabla ya Juni 20 mwaka huu.

Alisisitiza kuwa kila mtendaji aliyekabidhiwa vitambulisho hivyo, anapaswa kuvipeleka kwa wananchi katika vitongoji, mitaa, vijiji na kata zote na kuhamasisha kila mjasiriamali au mtoa huduma katika jamii kuwa na kitambulisho chake.

Mwanri aliwataka kuhakikisha kila mwananchi atakayelipia kitambulisho hicho, anajaza fomu maalumu na kuweka picha yake ili kuwa na kumbukumbu sahihi ya wajasiriamali na watoa huduma wote ikiwamo kujua biashara au huduma wanazotoa.

Aliongeza kuwa kuanzia sasa, sifa ya kwanza kwa mjasiriamali yeyote anayetaka kunufaika na mikopo inayotolewa na halmashauri ni kuwa na kitambulisho hicho, hivyo akawataka wakurugenzi wa halmashauri zote za Mkoa wa Tabora kutumia kigezo hicho katika utoaji mikopo na siyo vinginevyo.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) mkoani Tabora, Aniceth Anthon, aliyeambatana na mkuu wa mkoa huo kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuchangamkia fursa ya vitambulisho hiyo, alisema Sh. 20,000 wanayolipia kupata kitambulisho ni kwa ajili ya gharama za matengenezo ya kitambulisho hicho tu, hivyo akawataka wajasiriamali wadogo na watoa huduma wote kuhakikisha walipia na kupata kitambulisho hicho.

Pia, aliwahakikishia kuwa mtu yeyote atakayekuwa na kitambulisho hicho, atafanya biashara au kutoa huduma yoyote mahali popote pale nchini pasipo kubughudhiwa na mtu yeyote.

## Corona yatoa likizo ulipaji mikopo ya bil. 160/- Exim

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imetangaza msamaha wa likizo ya malipo ya mikopo kwa wateja wake wakubwa, wa kati na wadogo walipo katika sekta zilizo athirika zaidi kiuchumi kutokana na athari za mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya Covid 19.

Hatua hiyo ni sehemu ya juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na benki hiyo katika kuwasaidia kifedha wateja wake waliopo katika sekta ambazo zimeathiriwa zaidi na athari za mlipuko wa ugonjwa huo, unaosababishwa na virusi vya corona.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hii jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, msamaha huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 160 umeanza mwezi huu, ukihusisha likizo ya malipo ya mikopo kwa wateja na nyongeza ya muda wa urejeshaji wa mikopo ili kusaidia wateja wa benki hiyo katika sekta mbalimbali kutokana na athari za janga hilo kwenye biashara zao.

"Benki inaelewa mahitaji ya wateja wetu wakati huu na tunafanya yote yanayowezekana kuwasaidia ili waweze kuvuka salama katika kipindi hiki kigumu. Jitihada hizi haziishii tu kwenye misamaha hii tunayoitoa bali pia kupitia huduma za ushauri kuhusu mikakati ya biashara ili kuhakikisha kwamba biashara za wateja wetu zinadumu na zinafanyika kwa mafanikio zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Matundu, msamaha huo unazingatia vigezo mbalimbali kwa kila mteja kwa kuwa athari za Covid-19 hazikuwa sawa katika sekta zote. "Tunafarijika kwa kuwa tayari wateja waliopo kwenye sekta zilizoathiriwa zaidi wameshaanza kusaidiwa. Mazungumzo na wateja wengine bado yanaendelea ili kutambua hatua mbalimbali zinazofaa kulingana na aina ya biashara, " aliongeza.

"Siku zote Benki ya Exim, tunaamini katika kufanya kazi kwa bidii leo kwa ajili ya kesho bora kwa wateja wetu, biashara zao na jamii kwa jumla, ni kwa mtazamo huo tumepitisha hatua kama hii katika wakati huu mgumu. Tunaendelea kujitolea kushughulikia mambo haya na kupata suluhisho sambamba na mamlaka pamoja na serikali katika kuhakikisha uchumi wetu unaendelea kuwa thabiti wakati wa nyakati hizi ngumu," alisema.

# Tarehe ya msimu wa pamba yatajwa

**Na Mathias Canal, MWANZA**

SERIKALI imetangaza kwamba msimu wa ununuzi wa pamba wa mwaka 2020/2021 utazinduliwa Juni 2020.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitoa tangazo hilo, jana wakati akizungumza kwenye mkutano maalumu wa wadau wa tasnia ya pamba jijini Mwanza.

Alibainisha kuwa msimu wa pamba utazinduliwa wakati ambao serikali imejiweka kando kutopanga bei elekezi katika zao hilo pamoja na mazao mengine badala yake bei za mazao zitatokana na soko.

Alisema kuwa kazi ya serikali ni kuhakikisha kuwa inasimamia uzalishaji bora wa mazao na kusimamia upatikanaji wa masoko ya mazao ili kuwa na bei nzuri yenye manufaa kwa wakulima.

Alisema kuwa kutokana na usimamizi madhubuti wa serikali kupitia Wizara ya Kilimo, uzalishaji wa pamba umeongezeka kutoka tani 122,178 msimu wa ununuzi wa 2015/2016 hadi tani 348,910 msimu wa 2019/2020.

Waziri Hasunga alieleza kuwa zao la pamba ni mhimili wa uchumi wa wananchi wengi katika mikoa 17 na milaya 56 zinazozalisha zao hilo.

Kiwango kikubwa cha uzalishaji kwa miaka ya karibuni kilifikiwa katika msimu wa ununuzi wa 2011/12 ambapo kiasi cha tani 357,133 za pamba zilizalishwa.

Kutokea hapo, uzalishaji umekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka ambapo katika msimu wa kilimo wa 2015/16, uzalishaji ulikuwa tani 122,178 kiasi ambacho ni kidogo kuwahi kuzalishwa nchini.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani, hatua kadhaa za makusudi zimechukuliwa na Wizara ya Kilimo ili kulinusuru zao la pamba ambapo malengo ya wizara kwa sasa ni kuzalisha tani 1,000,000 za pamba ifikapo mwaka 2022/2023.

Alizitaja hatua zilizochukuliwa na serikali ni kuhamisha makao makuu ya Bodi ya Pamba kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza ili kuwa karibu na maeneo yanayolima pamba na kuwahudumia wakulima kwa karibu zaidi. Kutokana na hatua hiyo, ufanisi wa utendaji wa huduma kwa wakulima umeongezeka.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Changwa Mkwazu, akisoma taarifa ya baadhi miradi ya maendeleo kwa wananchi wa kata ya Nagaga (hawapo pichani) inayotekelezwa na serikali katika Kata ya Nagaga wilayani Masasi kwenye mkutano na wananchi hao jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Wanaoingiza maziwa nchini wasakwa

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa mwezi mmoja kwa maofisa wa serikali kuwasaka na kuwakamata watu wanaojihusisha na uingizaji wa mazao ya mifugo nchini, ikiwamo maziwa na kuwachukuliwa hatua kali za kisheria.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Maziwa yaliyofanyika Kitaifa jijini Dodoma kwa njia ya kielektroniki, Waziri Mpina alisema kamwe Tanzania haiwezi kukubali kugeuzwa soko la bidhaa zinazoingizwa kiholela kutoka nje ya nchi, huku akitaka hatua za kuimarisha uwekezaji nchini ziendelee kuchukuliwa.

Alisema suala hilo litasimamiwa kikamilifu na wizara yake ili kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Mpina alimwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo (DVS), Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko (DPM), Bodi ya Maziwa (TDB) na Bodi ya Nyama (TMB) kuongeza udhibiti kupitia Operesheni Nzagamba, ili kuzuia kwa namna yoyote uingizaji wa mazao ya mifugo nchini bila ya kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Pia aliagiza wanunuzi wote wa maziwa hasa wasindikaji kuzingatia mwongozo uliotolewa na wizara wa kununua maziwa ghafi kwa bei isiyopungua Sh. 800 kwa lita ya maziwa, ili kufidia gharama za uzalishaji, kuvutia uwekezaji na kuchochea uzalishaji zaidi kwa wafugaji.

Kadhalika, aliagiza kuzingatiwa bei elekezi ya Sh. 10,000 kwa uhimilishaji kwa ng'ombe bila vichochezi kama ilivyowekwa katika kanuni.

Alisema kanuni hizo zimetungwa ili kuweka usimamizi thabiti wa uhimilishaji nchini na kuweka bei elekezi ambayo inatoa unafuu zaidi kwa wafugaji badala ya kiwango cha zamani cha zaidi ya Sh. 25,000 kwa ng'ombe.

"Ninaagiza katika kipindi cha miaka miwili ijayo nchi yetu isiagize tena maziwa kutoka nje ya nchi, wadau wote wanaagizwa kuweka mikakati madhubuti kufikia malengo hayo," alisema Mpina na kuongeza:

"Nchi yetu ina ardhi yenye rutuba, ina malisho bora na mifugo mingi, hatuwezi kuendelea kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi. Tena wakati mwingine tunaagiza maziwa kutoka nchi ambazo hazina hata mifugo, suala hili halivumiliki tena," alisema Waziri Mpina.

Alisema wizara imepokea maelekezo kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kupitia Mwenyekiti wake, Mahmoud Mgimwa, kupiga marufuku matumizi ya maziwa ya unga kama NIDO, Lactogen kutoka nje ya nchi katika ofisi za serikali.

Alisema suala hilo litasimamiwa kikamilifu na Wizara ya Mifugo ili kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. Sophia Mlote, alisema wiki ya maziwa imeleta hamasa kubwa kwa wananchi na kumhakikishia Waziri Mpina kuwa atasimamia maelekezo yote ili kuleta mageuzi ya kweli kwenye sekta ya maziwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Wadau wa Maziwa, Catherine Dangat, aliishukuru serikali kwa hatua inayochukua ya kudhibiti uingizaji holela wa maziwa kutoka nje ya nchi na kuomba udhibiti huo uendelee ili kulinda viwanda vya ndani.

# Hanang' yaanza kutekeleza agizo la JPM

**Na Daniel Sabuni, KATESH**

SERIKALI wilayani Hanang' mkoani Manyara, imeanza kutekeleza agizo la Rais John Mgufuli la kuwataka wakulima kuhifadhi mavuno ya zao la mahindi na kutouza bei ya chini ili wasubiri bei itakapopanda.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Joseph Mkiriti, alisema kuwa wamepokea maagizo hayo kwa umakini mkubwa na kuanza kujadili kwa pamoja katika ngazi ya wilaya.

"Tumekutana na viongozi wanaokutana na wananchi wetu moja kwa moja, kama madiwani na viongozi wa kata, vijiji na kutekeleza kwa jinsi gani tunafikisha agizo hili kwa wananchi, viongozi watalifikisha kwenye mikutano yao ya vijiji na mitaa kwa namna watakavyoona inafaa, huku wakichukua tadhari ya ugonjwa wa corona," alisema Mkiriti.

Alisema agizo la Rais Magufuli limetolewa wakati muafaka kwa sababu uvunaji wa mahindi ndiyo unafanyika wilayani humo.

"Tutawafikishia maono haya ya Rais Magufuli kama mwananchi anavuna gunia 50 auze hata 10 atatue changamoto za mahitaji ya familia halafu ahifadhi, hivi sasa gunia la mahindi lenye debe sita ni Sh. 45,000 lakini mwaka huu mwanzoni tumeshuhudia likiuzwa Sh. 120,000," alisema Mkiriti.

Alisema hali ya mavuno kwa Wilaya ya Hanang' mwaka huu inaonyesha kutia moyo kwani wakulima wana matarajio ya kuvuna kisi cha tani 124,199 za mahindi.

Alisema kwenye zao la maharage mwaka huu wamepata mavuno kidogo ya tani 747.8 tofauti na malengo waliyojiwekea ya kuvuna tani 19358.7.

"Tumewaambia tutunze mavuno yetu kwa usalama wa mlaji, lakini kuweka thamani ya mnunuzi, ukitunza vizuri unakuwa na uhakika wa bei," alisema Mkiriti.



# Brela yaeleza safari kwenda kidijitali

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Leseni na Biashara (Brela), imefanikiwa kutengeneza mifumo ya kisasa ya usajili wa leseni na biashara inayofanyakazi bila watu kulazimika kufika kwenye ofisi zake.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Godfrey Nyaisa, wakati akihojiwa na moja ya televisheni kuhusu mageuzi ambayo ameyafanya kwenye taasisi hiyo miezi minne bada ya kuteuliwa.

Nyaisa alisema hivi sasa wamepunguza kwa asilimia 80 idadi ya watu wanaofika kwenye ofisi hizo kwani shughuli zote zinafanyika kwa mtandao ambao umerahisisha upatikanaji wa leseni na kuondoa malalamiko.

"Tumepunguza watu kuja ofisini kwetu kwa sababu kuonana onana pale ndiko kulisababisha mianya ya rushwa, lakini sasa ni mfumo kwa mfumo, mtu kama ana jambo anatuma barua pepe inajibiwa hapohapo na mimi CEO kila kinachoingia naona na kimefanyiwa kazi na nani," alisema Nyaisa.

Nyaisa alisema kila siku asubuhi mtu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Brela (IT) humpa taarifa kuhusu kazi zilizofanyika kwa siku, hali ambayo inamsaidia kuwabaini watumishi wasiowajibika kwenye nafasi zao.

"Kwa mifumo tuliyoiweka mtu wa IT ananipa kila kitu kwamba mtumishi huyu aliingia kwenye mfumo saa ngapi na ameshughulikia kazi ngapi kwa siku hiyo sasa hapo wale watumishi wavivu ni rahisi sana kuwabaini," alisema Nyaisa.

Nyaisa alielezea mkakati mwingine wa kuendelea kuisuka upya Brela kuwa ni kuwatengeneza sare watumishi wote wa taasisi hiyo, ili kuleta nidhamu na kuheshimiana miongoni mwa watumishi badala ya utaratibu wa sasa wa kila mtu kuvaa anavyotaka yeye.

Nyaisa alisema sare itasaidia pia kuwabaini watumishi vishoka ambao wamekuwa wakiwadanganya watu kwamba ni watumishi wa taasisi hiyo na kuwaibia fedha zao.

**"Kwa mifumo tuliyoiweka mtu wa IT ananipa kila kitu kwamba mtumishi huyu aliingia kwenye mfumo saa ngapi na ameshughulikia kazi ngapi kwa siku hiyo sasa hapo wale watumishi wavivu ni rahisi sana kuwabaini," alisema Nyaisa.**

# Waziri atoa matumaini Vitambulisho vya Taifa

**Na Augusta Njoji, MPWAPWA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema hivi karibuni mitambo mipya ya uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa itaanza kufanya kazi baada ya wataalamu kutoka Ujerumani kuwasili nchini.

Mitambo hiyo ilitakiwa kuanza kufanya kazi, Aprili 30, mwaka huu, lakini imechelewa kuanza kutokana na ugonjwa wa corona na kutawezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kutoa vitambulisho 180,000 kwa siku.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Malolo na Ipela, jimboni kwake Kibakwe, Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, alipokuwa akipongezwa kwa kuchaguliwa kuiongoza wizara hiyo.

Alisema mitambo hiyo imenunuliwa kutoka Ujerumani na wataalamu walishindwa kuja Tanzania kutokana na nchi hizo kufunga anga kwa sababu ya corona.

"Hivi sasa serikali imefungua ili ndege zingie na wataalamu watakuja wakati wowote na wakishatengeneza tutahakikisha tunaanza uzalishaji wa haraka wa vitambulisho na Watanzania wako tayari kupata kitambulisho kwa kila mmoja anayesubiri," alisema.

Aliongeza: "Kwa sasa tulikuwa na uzalishaji mdogo wa vitambulisho kwa sababu mitambo yetu ilikuwa imepata hitilafu, lakini tumefunga mitambo mipya ambayo kwa siku itatoa vitambulisho kama 140,000 ukiunganisha na ile ya zamani hivyo itakuwa 180,000 kwa siku moja."

Aliuhakikishia umma kuwa kama NIDA watatoa kwa idadi hiyo anauhakika wananchi wote waliojisajili watapata na hata wapya wanaoendelea kujisajili.

Alisisitiza tatizo la vitambulisho vya Taifa linaenda kwisha mapema iwezekanavyo na litakuwa ni historia.

Akizungumzia utendaji wa Rais John Magufuli, Waziri Simbachawene alisema serikali anayoiongoza imefanya kazi iliyotukuka ndio maana upinzani unakufa wenyewe.

"Sasa hivi unaona kuna Chadema huku? Hata huko mjini haupo, kama ni ugomvi ni ugomvi wa watoto wa nyumba moja, hakuna upinzani kwa sasa mnasikia watu wanahama wanaenda CCM wengine huku, ni kwa sababu ya kishindo cha kazi kilichofanywa na serikali chini ya Rais Magufuli," alisema.

Alisema wanaenda kwenye uchaguzi wa mchujo wa CCM kwa upole kwa kuwa hakuna haja ya kutoka jasho na wagombea wao watashinda dhidi ya vyama vya upinzani.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Kikao hicho, Emmanuel Kagali, alimwomba waziri huyo kuwasaidia kupata vitambulisho vya Taifa, kwani idadi kubwa ya wananchi wa Kata ya Malolo hawajapata bado.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha (wa pili kulia), akimkabidhi msaada wa godoro, blanketi, ndoo ya maji na chandaruwa Ilyeto Samige mkazi wa kata ya Nganya, Hamashauri ya Msalala, aliyepata maafa jana, msaada huo ulitolewa na Shirika la Tanzania Redcross Society kwa ajili ya kaya 266 zilizopata maafa. **PICHA NA SHABAN NJIA**

# Waliolima hifadhini wapewa siku 30

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ametoa mwezi mmoja kuanzia jana kwa wakulima wote waliokuwa wamelima mazao yao katika Msitu wa Hifadhi ya Makere Kusini uliopo wilayani Kasulu kuvuna na kuondoa mazao yao na baada ya hapo watakaolima tena watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alitoa agizo hilo jana mkoani Kigoma katika Wilaya ya Kasulu wakati alipokuwa akizungumza na watumishi wa TFS pamoja na viongozi wa CCM wa wilaya hiyo.

Hatua hiyo inakuja kufuatia malalamiko kutoka kwa wakulima wanaodai kunyang'anywa mazao yao ikiwa pamoja na kunyanyaswa na maofisa misitu wakati wanapokuwa wanapita wakiwa katika njia inayokatisha ndani ya msitu huo.

Alisema sio busara kusubiri kumkata mkulima ambaye amelima akaachwa akapalilia mazao yake akaacha, ila baada ya kuanza kuvuna mazao yake ndipo anaanza kukamatwa na kulipishwa faini.

Alisema kitendo cha kukamata mazao ya wananchi yakiwa yameshavunwa ni kuwasababishia njaa na umaskini.

Kanyasu amevitaka vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na TFS kuwadhibiti na kuwachukulia hatua kali za kisheria wakulima ambao ni Watanzania wanaotoa kazi za vibarua ambao ni raia wa Burundi kulima ndani ya msitu huo.

Aliiitaka TFS kuwakamata vibarua hao ambao sio raia wa Tanzania na kuwapeleka mahakamani hatua ambayo itasaidia kuwataja Watanzania wanaotoa vibarua vya kulima katika msitu huo kwa wageni.

Kwa upande Mbunge wa Kasulu Vijijini, Vuma Ole, alisema hatua ya kuwaruhusu wananchi kuvuna mazao yao itasaidia kupunguza uhasama uliopo kati ya wakulima na wahifadhi.

Hata hivyo, aliitaka TFS kusimamia msitu wa Makere kipindi chote na sio kipindi cha mavuno pekee kwani hali hiyo inashawishi mazingira ya rushwa.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Simon Anange, alisema baada ya kuchunguza malalamiko yanayotolewa na wananchi imebainika kuwa wakulima wengi wanaolima katika msitu huo ni raia wa Burundi na sio Watanzania kama inavyodaiwa.

Kutokana na hali hiyo, Kanali Anange amewaonya Watanzania wanaowakaribisha raia wa Burundi na kuwapa vibarua vya kulima katika msitu huo waache mara moja. Kwa upande wake, Mhifadhi Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, aliwataka wananchi kufuata sheria kwa kuacha kulima katika msitu huo kwani ni kosa kisheria.

# Biteko aipa 5 GGML uwekezaji kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameipongeza kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu - Geita (GGML) kwa kuwa mdau wa mfano katika kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Geita.

Biteko ametoa kauli hiyo katika ziara mkoani Geita na kukagua miradi inayotekelezwa na GGML chini ya mpango wake wa kusaidia jamii (Corporate Social Responsibility) katika Mji wa Geita.

"Nimefurahishwa na namna ambavyo serikali katika Mkoa wa Geita inavyosimamia ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye sekta ya madini. Tayari tumeshafikia lengo la kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 400 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni mwaka huu kutoka kwenye sekta hii, na sehemu kubwa ya makusanyo haya imetoka Geita, hususani GGML.

"Inatia moyo sana kuona kwamba sekta hii sasa inachangia zaidi ya asilimia 5 ya uchumi wa nchi yetu. Lengo ni kuhakikisha kwamba sekta ya madini inachangia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025," alisema Biteko.

Mojawapo ya miradi ambayo ilikaguliwa na waziri huyo katika ziara yake ni ujenzi wa Kanda maalumu ya uwekezaji 'Special Economic Investment Zone' ambao utasimamiwa na Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji (EPZA) na Halmashauri ya Mji wa Geita.

Pia alitembelea miradi mingine ya kimkakati inayofadhiliwa na GGML, ikiwamo ujenzi wa Soko Kuu la Geita Mjini na soko la Katundu.

Makamu wa Rais anayeshughulikia Maendeleo Endelevu katika Kampuni ya GGML, Simon Shayo, alisema utekelezaji wa miradi ambayo imetembelewa na Biteko ni sehemu ya mpango wa mwaka 2018/19 unaoenda sambamba na mojawapo ya tunu za kampuni hiyo inayoelekeza kwamba jamii inayozunguka shughuli zake sharti ifaidike kwa uwepo wake.

Alisema GGML inawajibika ipasavyo kwa jamii kwani hutumia Sh. bilioni 9.2 kila mwaka kugharamia miradi ya jamii katika mkoa wa Geita na kuifanya kampuni hiyo kuwa ya kipekee kutokana na mchango mkubwa inayotoa kusaidia jamii.

"Kama kampuni-raia ndani ya Tanzania, GGML iliyoko chini ya Anglo-Gold Ashanti itaendelea kuunga mkono na kusaidia jamii zinazotuzunguka. Utekelezaji wa miradi ya CSR na shughuli zingine kama hizo ni ushahidi wa wazi kwamba kampuni, serikali na jamii zikifanya kazi pamoja zinaweza kuboresha maisha ya watu kupitia uwekezaji endelevu katika miundomuni ya biashara na huduma.

"Tunataka kuona maisha ya mtu wa kawaida katika jamii yetu yakiwa bora zaidi kupitia uwekezaji endelevu wa kampuni yetu" alisema.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2018, GGML iliwezesha utekelezwaji wa miradi kadhaa kupitia mpango wake wa kuwekeza katika jamii.

"Miradi hii inajumuisha; uwekaji wa taa za barabarani katika mji wa Geita, ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti, ujenzi wa soko la kisasa Geita mjini, umaliziaji wa majengo zaidi ya 600 ya afya na elimu na ujenzi kamili wa shule tatu mpya na vituo vya afya vinne.

"Pia GGML imetenga kiasi cha Sh. bilioni 18 kwa ajili ya miradi mingine kama hiyo katika kipindi cha kati ya mwaka 2019/20 na 2020/21.



Makamu wa Rais anayeshughulikia Maendeleo Endelevu katika Kampuni ya GGML, Simon Shayo, akizungumza katika ziara ya Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliyetembelea miradi ya kampuni hiyo inayotekelezwa chini ya mpango wa kusaidia jamii (CSR) mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Mara ataka mil. 50/- zirudishwe

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, amesikitishwa na kitendo cha wataalamu wa idara mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kutokuheshimu maazimio yanayotolewa na madiwani, likiwamo azimio la Sh. milioni 50 za makusanyo ya ndani kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi.

Aliyasema hayo kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani kujadili hoja za ukaguzi na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Malima alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Amosi Kusaja na wakuu wa idara kuwa ifikapo Juni 30, mwaka huu, wawe wamerudisha fedha za maendeleo Sh. milioni 50, pamoja na mashine sita za kukusanyia mapato zilizopotea kwa kile kinachoelezwa kuwa ni uzembe wao.

"Mkurugenzi na wataalamu wako hamuwaheshimu madiwani na ndiyo maana mnafanya mambo yao tu na si kwa kufuata maazimio ya madiwani. Lakini ninawaomba msiwe wadanganyifu," alisema Malima.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Coroline Mthapula, alisema wakuu wa idara hawatoi ushirikiano wa kutosha kwa mkaguzi wa ndani, ikiwa ni pamoja na kutokujibu hoja za ukaguzi kwa wakati.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alisema wakuu wa idara ni wazembe kwani wanaacha rasilimali za serikali zinapotea.

## KWA UFUPI

### Kesi 80 zaripotiwa uharibifu mazingira

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

KATIKA kupambana na vitendo vya uharibifu wa mazingira, kesi 80 zimeripotiwa katika Idara ya Misitu na mali zisizorejesheka kisiwani Pemba kuanzia Januari hadi Desemba 2019.

Ofisa doria wa idara hiyo, Rashid Suleiman Rashid, alieleza kuwa kati ya kesi hizo ni kesi 64 tu ndizo ambazo zilizoshatolewa uamuzi, huku kesi 14 zikiwa katika vituo vya Polisi na hazijasikilizwa wakati kesi 1 tu ikiwa iko mahakamani.

Alisema kesi ambazo zimesikilizwa ni ambazo watuhumiwa walikubali wenyewe kesi zao zisikilizwe idarani kwao, kwani ofisi yao imepewa mamlaka ya kufanya hivyo.

Katika mwaka 2019 tuliweza kufanya doria 55 na tukafanikiwa kupata kesi 80, kati ya hizo kesi 65 tu ndizo zimepatiwa ufumbuzi, ambapo kesi ni zile ambazo watuhumiwa wake walikubali kesi zao zisikilizwe idarani kwetu kwa mujibu wa sheria, kesi 14 bado ziko katika vituo vya Polisi Wete, Mchangamdogo, Chakechake, Mkoani huku kesi 1 tu ndio iliyoko mahakamani," alisema Rashid.

"Pia tumekuwa tukipambana na watumiaji wa misumeno ya moto (chelsoo), ambapo kwa mwaka 2019 jumla ya misumeno saba tulifanikiwa kuikamata na tunapoikamata tu pale pale tutaitaifisha."

### Wateja SBL Kanda Ziwa wakumbukwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya bia ya Serengeti (SBL) imezindua bia mpya ya Pilsner Lager yenye ujazo wa mililita 300 mahususi kwa ajili ya wateja wake wa eneo la Kanda ya Ziwa.

Kinywaji hicho maarufu kama 'Bia Imara kama Simba' itakuwa ikipatikana katika eneo lote la Kanda ya Ziwa.

"Wakazi wa eneo hilo wanafahamika kwa sifa yao ya uchapa kazi. Bia hii ambayo ni mahususi kwa ajili yao, sasa inapatikana katika eneo lote la kanda ya ziwa kwa ajili ya kuwaburudisha wakazi wa eneo hili baada ya kazi za kila siku kwa shilingi 1,000 tu," alisema Anitha Msangi, Mkuu wa Kitengo cha bia wa SBL

Kampuni ya SBL ambayo ndiyo mzalishaji wa Pilsner, pia ndiyo mzalishaji wa bia yenye kimea kwa asilimia 100, Serengeti Premium Lager pamoja na bia laini maarufu yenye chimbuko lake hapa nchini Serengeti Lite. SBL pia ni wasambazaji wa vinywaji kama Johhnie Walker, Ciroc, Smirnoff Vodka, White Horse J&B na nyinginezo.

Nipashe
# Spotika



NYOTA WA5 MAN UNITED WA KUTHIBITISHA UBORA UK. 12&13



HAKIMI

# 5-BORA WA MKOPO ULAYA MSIMU HUU

**LONDON,** England

USAJILI wa mkopo unaweza kutumika zaidi katika dirisha la usajili linalokuja kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Umekuwa msimu wa mkopo kwa wachezaji wakubwa msimu huu. Moja wapo ni Phillipe Coutinho kutoka Barcelona kwenda Bayern Munich na Alexis Sanchez kutoka Manchester United kwenda Inter Milan. Bahati mbaya hawa hawajawa kwenye kiwango cha kuvutia. Wameshindwa kuonyesha makali yao kwenye timu wanazozichezea, hivyo usajili wao unaonekana kutokuwa na mafanikio.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji watano wanaocheza kwa mkopo ambao wana mafanikio zaidi barani Ulaya msimu huu...

**#5. CHRIS SMALLING**

Chris Smalling amecheza sana pale Manchester United, lakini mwaka jana alionekana kutokuwa kwenye kiwango. Hivyo, wakati United walipomsajili Harry Maguire kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia, mkongwe huyu alipelekwa AS Roma kwa mkopo.

Kila mmoja alifikiria kwamba hiyo itakuwa biashara mbaya kwa Roma, lakini Smalling amethibitisha ubora wake. Muingereza huyu amekuwa mmoja wa viongozi wa timu na amekuwa na msimu mzuri sana katika kila mechi kule Italia msimu huu.

**#4. MAURO ICARDI**

Ni mchezaji mtata wa Argentina, Mauro Icardi, na alikuwa nyota pale Inter Milan kwa kipindi cha miaka kadhaa. Lakini msimu huu akapelekwa PSG wakati Inter ikijengwa upya. Zuri zaidi kwake ni kwamba amefanikiwa kuwa mmoja wa washambuliaji watatu wa PSG na kumweka benchi Edinson Cavani.

Icardi ana mabao 20 msimu huu; huku tayari PSG ikiwa imefuzu kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, anatarajiwa kufunga zaidi. Na tayari PSG wameamua kumsajili kwa mkataba wa kudumu.

**#3. DEAN HENDERSON**

Mwaka mmoja uliopita, Dean Henderson alikuwa mchezaji wa mkopo wa Manchester United. Kwa sasa ni mmoja wa magolikipa wenye nafasi kubwa zaidi katika kikosi cha timu ya Taifa ya England.

Amekuwa akitajwa kama mmoja wa makipa bora zaidi wa Ligi Kuu ya England msimu huu na amecheza mechi 10 za ligi bila kuruhusu bao. Chini ya kocha, Chris Wilder, Henderson ana nafasi kubwa zaidi ya kucheza kwenye mashindano ya mataifa ya Ulaya mwakani hasa kutokana na mafanikio yake kule Sheffield United.

**#2. MARTIN ODEGAARD**

Real Madrid walimsajili wakati akiwa na umri wa miaka 15, raia huyu wa Norway, Martin Odegaard. Akacheza kwa mkopo katika misimu mitatu na sasa yupo tayari kucheza katika kikosi cha kwanza.

Alikuwa na wakati wa kuvutia kipindi akicheza kule Vitesse na Heerenveen nchini Uholanzi, na msimu huu anaonyesha kiwango chake kule Real Sociedad.

Odegaard pengine ndiye kiungo mshambuliaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu huu na amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa Sociedad. Kwake yeye Real Madrid wamemtengeneza mrithi wa Luka Modric.

**#1. ACHRAF HAKIMI**

Achraf Hakimi ni mchezaji wa Real Madrid ambaye amekuwa na msimu wa kuvutia sana. Hakimi kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Borussia Dortmund, na mwishoni mwa msimu huu ataweza kurudi Madrid.

Hakimi tayari ameshajijengea heshima yake kama mmoja wa mabeki bora zaidi wa kulia duniani. Akiwa kule kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundelisga, Hakimi amekuwa nguzo kuu ya timu.

Hakimi upatina wake na Raphael Guerrero pale Borussia Dortmund umetengeneza kitu cha kuvutia sana. Na kule Real Madrid, anaonekana ndiye mrithi wa mkongwe Dani Carvajal.

## ISIKUPITE

ROBERT Lewandowski juzi alikuwa miongoni mwa wafungaji wakati Bayern Munich ikishinda 4-2 dhidi ya Bayer Leverkusen, hilo ni bao lake la 30 kwenye Bundesliga msimu huu na la 44 katika mashindano yote msimu huu, hivyo amebakiza mechi tatu tu kuipigania rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao 40 kwa msimu mmoja kwenye Bundesliga.



## Extra Time



DAVID DE GEA

# NYOTA WA5 MAN UNITED WA KUTHIBITISHA UBORA

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United haipo kama vile ilivyozoeleka. Anguko lao linajulikana wazi kwa kipindi cha miaka sita na nusu tangu kuondoka kwa Sir Alex Ferguson.

**Kutoka kuwa mabingwa wa Ligi Kuu England chini ya usimamizi wa raia huyo wa Scotland, Man United imemaliza mara mbili tu ndani ya nne bora tangu kuondoka kwake na imetupwa kando na timu kama Manchester City na Liverpool.**

Man City imechomoza na kuwa inayocheza soka la kisasa chini ya Pep Guardiola, huku ikishinda mataji mawili ya Ligi Kuu.

Liverpool pia imeimarika chini ya Jurgen Klopp na imetwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku pia ikitawala msimu huu wa ligi.

Man United kwa sasa wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi na wapo pointi tatu nyuma ya Chelsea waliopo nafasi ya nne. Na walijikuta wakiwa kwenye kiwango bora na hawakufungwa katika mechi 11 wakati msimu uliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Klabu sasa zimeruhusiwa kurudi kwenye mazoezi na Ligi Kuu ya England ikitarajiwa kurudi baadaye mwezi huu.

Katika hilo, tunawaangalia wachezaji watano wa Man United ambao wana kitu cha kuthibitisha wakati Ligi Kuu itakapoanza tena:

### # 5: HARRY MAGUIRE

Ni mlinzi wa kati ghali zaidi wa wakati wote, Harry Maguire hajafurahia kiwango chake tangu alipompiku Virgil Van Dijk kwenye rekodi ya beki bora.

Ubora wa Maguire kama beki na kiongozi kwenye vyumba vya kubadilishia nguo umekuwa ukisifiwa na kocha wa Man United, Solskjaer, ambaye alimteua kama nahodha. Lakini kiwango chake kinaonekana kushuka tofauti na alipotua hapo akitokea Leicester.

Man United imeruhusu mabao machache chini ya uwepo wa Maguire. Lakini bado kunaonekana udhaifu kwa klabu katika ulinzi.

Maguire anayeshikilia rekodi ya usajili ghali zaidi wa beki duniani hajatimiza matarajio ya wengi. Sasa ni suala lake yeye mwenyewe kuonyesha thamani yake.

### # 4. ERIC BAILLY

Bahati mbaya ni kwamba, Eric Bailly hajacheza zaidi ya mechi 30 kwenye Ligi Kuu England akiwa na Manchester United kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita.

Mlinzi huyu wa kati raia wa Ivory Coast alipewa nafasi kubwa zaidi chini ya Jose Mourinho. Alikuwa mchezaji muhimu zaidi wa kikosi cha kwanza cha Manchester United katika msimu wake wa kwanza wa 2016/17 wakati alipocheza mechi 39 katika mashindano yote.

Hata hivyo, majeraha yamekuwa adui mkubwa wa Bailly na kumfanya muda mwingi kuwa nje ya dimba. Majeraha yamekuwa mabaya zaidi kwa Bailly msimu huu na hajawa kwenye kikosi cha Man United kwa muda mrefu.

Bailly alionyesha kiwango cha kuvutia dhidi ya Chelsea wakati Man United wakicheza ugenini pale Stamford Bridge. Mechi ile ilikuwa moja kati ya mara mbili alizoichezea klabu hiyo kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Huku kukiwa na matatizo ya kifedha kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, Bailly anaweza kuwa mtu ambaye Man United inaweza kumtoa hasa kutokana na majeraha pamoja na mshahara wake, isipokuwa akionyesha kiwango chake kama alivyocheza dhidi ya Chelsea pale Stamford Bridge.

### # 3. LUKE SHAW

Luke Shaw haonekani kama ni mchezaji ambaye ana umri wa miaka 24. Mara ya kwanza alikuwa akichukuliwa kama mmoja wa mabeki bora zaidi wa kushoto wanaoibukia kwenye soka. Lakini maendeleo ya Shaw pale Man United yamekuwa sawa na mchezaji mwenzake, Eric Bailly ambaye amekuwa anasumbuliwa na majeraha tangu enzi za Jose Mourinho.

Akiwa ametoka kwenye akademi ya soka ya Man United, Shaw anaonekana hayupo kabisa kwenye mipango ya Ole Gunnar Solskjaer na kipaji chake kinaonekana kudidimia.

Hata hivyo, mengi yapo yakumpongeza Shaw kwa nafasi yake aliyoisaidia Man United wakati ikicheza mechi 11 bila kufungwa kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19.

Shaw sasa anahitaji kujiimarisha yeye mwenyewe na pia kuwa fiti ili kupata namba ya kudumu katika kikosi cha Man United.

### # 2. DAVID DE GEA

Mshindi mara nne wa tuzo ya mwaka ya Matt Busby na awali alichukuliwa kama golikipa bora zaidi duniani. David de Gea ameshuka kiwango msimu huu.

De Gea hivi karibuni alishuka kutoka kuwa golikipa namba moja wa Hispania na nafasi yake ikichukuliwa na kipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga. Kipa huyo msimu huu hajaruhusu bao katika mechi nane tu kati ya 29 kwenye Ligi Kuu, huku akifanya makosa mengi sana langoni mwake na kuigharimu timu.

Mashabiki wa klabu hiyo watakuwa na matumaini ya kumwona akibadilika kiwango chake kwa kipindi cha msimu kilichobaki.

Nafasi yake inatishiwa na Dean Henderson ambaye amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kule Sheffield United ambako anacheza kwa mkopo msimu huu akiwa hajaruhusu bao katika mechi kumi kati ya 27.

De Gea anahitaji kuimarika kama anataka kuendelea kuwa na kiwango cha kuvutia zaidi na kuendelea kuibeba Man United, vinginevyo nafasi inaonekana kuwa wazi kwa Henderson kuchukua mikoba yake.

### # 1. PAUL POGBA

Raia huyu wa Ufaransa, Paul Pogba, amehusika katika mechi nane tu za Manchester United kwenye mashindano yote msimu huu. Lakini bado anapamba sana vyombo vya habari kuliko mchezaji yeyote katika timu hiyo.

Amekuwa akihusishwa sana na kutakiwa na klabu ya Real Madrid na pia timu yake ya zamani Juventus. Kocha wake, Solskjaer, anaonekana wazi kwamba hana mpango wa kumuuza Pogba. Lakini kutokana na matatizo ya kifedha yaliyosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, anaweza kufikiriwa kuuzwa.

Huu ni wakati wa Pogba kujaribu kuonyesha kipaji chake ili kujiimarisha zaidi kama mmoja wa viungo bora zaidi duniani.

Itakuwa ni ngumu kwa United kumwachia aondoke, kwa sababu wanajua kwamba bado ni mchezaji ambaye wanamhitaji zaidi.

Lakini Pogba lazima athibitishe kiwango chake ili kuendelea kuaminiwa na mashabiki wa Manchester United.

## Nukuu

"Sidhani kama soka litakuwa kama lile tulilolizoea, lakini licha ya soka, sidhani kama maisha kwa ujumla wake yatakuwa sawa tena. Sisi wote tuna uzoefu kwamba kwa hali hii mambo yatabadilika na tutakumbuka namna ilivyotokea kwa namna moja au nyingine, kwa upande wangu, nahisi huzuni hasa kwa wale waliopoteza ndugu zao kutokana na janga hili la corona," **mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi akizungumza na El Pais.**




"[Philippe Coutinho] ana mpango wa kurudi Ligi Kuu England, inaweza isitokee mwaka huu, lakini inaweza kutokea, hatuwezi kujua, hatujajadiliana kitu chochote kwa sasa," **wakala wake, Kia Joorabchian akiiambia Sky Sports.**



"Sina uhakika kama yeye [Kylian Mbappe] ni aina ya mchezaji ambaye atafiti kwenye mipango ya Jurgen Klopp, sioni uwezekano huo, angalau [Timo] Werner au [Jadon] Sancho wanaweza kufiti, lakini si kwa Mbappe, hafiti kabisa pale," **mchezaji wa zamani wa Liverpool, Jason McAteer akiiambia Stats Perform News.**



# KILA MTU NAASHINDE MECHI ZAKE LIGI KUU



Beki wa Yanga, Kelvin Yondani akiwa mazoezini kujiandaa na mechi za Ligi Kuu. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

JUMAMOSI ijayo, rasmi Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea na mechi zake zilizobaki kumalizika msimu wa 2019/20, baada ya kusimama tangu Machi 17, kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

**Ugonjwa huo uliosambaa duniani kote, ulisababisha ligi nyingi kuvunjwa na zingine kusimamishwa, huku Ujerumani ikiwa nchi ya kwanza duniani kurejesha ligi yake.**

Hapa Tanzania, baada ya kazi kubwa ya udhibiti wa ugonjwa huo na wagonjwa kupungua, hatimaye serikali imerejesha tena michezo, ikiruhusu pia ichezwe nyumbani na ugenini kama ilivyokuwa awali, badala ya vituo kama ilivyotaka kufanyika.

Pia, Ligi hiyo itachezwa na mashabiki, badala ya kuchezwa uwanja mtupu kama ilivyopendekezwa mwanzo. Hata hivyo, mashabiki watakaoingia watatakiwa kufuata taratibu zote zinazotakiwa kiafya.

Tukirudi kwenye mitanange yenyewe ni kwamba timu zote zinakwenda kumalizia michezo yao zilizobakisha ili kujua hatima yao. Tayari Bodi ya Ligi imeshatoa ratiba na kila timu inakwenda kucheza mechi yake ambayo huenda ikatoa mwelekeo wa kule inakotarajiwa kuwa.

Hata hivyo, zitaanza mechi tano za viporo kwanza, kabla ya ligi hiyo kusonga mbele. Makocha wengi wameonyesha kutoridhika na hali ya utimamu wa miili ya wachezaji wao, hivyo wanapambana kurekebisha hali hiyo.

Hii ina maana mechi za mwanzo zinaweza kutoa matokeo yasiyotarajiwa na kila timu inatakiwa ipambane na hali yake iliyokuwa nayo na kila mtu akitaka kuwa kwenye na hali nzuri ni lazima ashinde mechi zake.

Hizi ndizo mechi tano za viporo zitakazochezwa kuanzia Jumamosi na tathmini zake, kabla ya mechi zingine kuendelea kama kawaida.

**1. MWADUI VS YANGA (UWANJA WA KAMBARAGE)**

Mechi hii ndiyo itakuwa ya ufunguzi baada ya corona na itachezwa kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga Juni 13, ikiwa ni moja kati ya mechi mbili siku hiyo.

Ni mechi ya mzunguko wa kwanza, iliyopaswa ichezwe kwenye raundi ya 17, kwani Yanga haijacheza na Mwadui hata mechi moja. Inatarajiwa kuwa kali na ya kusisimua kwa sababu wenyeji huwa kama mbogo wanapokuwa kwao.

Yanga itaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa, ikikumbuka kuwa watani zao wa jadi kwenye uwanja huo huo walichakazwa bao 1-0, Oktoba 30, mwaka jana, ikiwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu.

**2. COASTAL UNION VS NAMUNGO (UWANJA WA MKWAKWANI)**

Juni 13 kwenye Uwanja wa Mkwakwani kutakuwa na kipute kingine cha ufunguzi kati ya wenyeji Coastal Union dhidi ya Namungo FC kutoka Ruangwa mkoani Lindi.

Ni moja ya mechi za kusisimua ya kiporo cha raundi ya 29, pia ya kisasi. Ikiwa ugenini, Namungo itakuwa na kazi ya ziada kutaka kulipa kisasi cha kufungwa mabao 3-1 nyumbani mechi ya mzunguko wa kwanza, Novemba 22, mwaka jana. Hata hivyo, timu zote haziko eneo salama kwenye msimamo wa ligi.

**3. SIMBA VS RUVU SHOOTING (UWANJA WA TAIFA)**

Mabingwa watetezi Simba kwa mara ya kwanza wataingia uwanjani Jumapili, Juni 14, wakiwa na mkakati wa kutaka kuchukua ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo dhidi ya Ruvu Shooting, ikiwa ni mechi ya raundi ya 29.

Haitokuwa mechi rahisi kwa Ruvu Shooting ambayo ina rekodi mbovu inapocheza na Simba, tena wakati mwingine ikipoteza kwa idadi kubwa ya mabao.

Hata, msimu huu zilipokutana kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, Novemba 23, Simba ilitandika Ruvu Shooting mabao 3-0, hivyo itakuwa na kazi ngumu ya kubadilisha rekodi hiyo.

**4. AZAM FC VS MBAO FC (UWANJA WA AZAM COMPLEX)**

Azam itakuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Azam Complex kucheza dhidi ya Mbao FC kutoka mjini Mwanza mechi ya raundi ya 29. Utakuwa ni usiku mgumu kwa Mbao, ambayo inapigana kufa na kupona kuhakikisha inabaki Ligi Kuu.

Timu hiyo ambayo haiko kwenye nafasi nzuri, ikishikilia nafasi ya 19, itakabiliana na timu ambayo bado inasaka ubingwa, lakini ikijiweka sawa na Kombe la FA. Huenda bahati nzuri kwa Mbao ni Azam kutokuwa na baadhi ya wachezaji wake tegemeo ambao wamekwama nchini kwao kutokana na karantini ya virusi vya corona. Mechi ya kwanza iliyochezwa Novemba 23, Uwanja wa Mkwakwani, Azam ilishinda kwa bao 1-0.

**5. JKT TANZANIA VS YANGA (UWANJA WA JAMHURI)**

Yanga itasafiri hadi Mji Mkuu Dodoma kucheza dhidi ya JKT Tanzania Uwanja wa Jamhuri kwenye mechi ya kiporo raundi ya 29. Ni moja kati ya mechi mbili za viporo za Yanga ilizokuwa nazo.

Rekodi inaturudisha nyuma kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, Yanga ilipoichapa JKT Tanzania mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Novemba 22, mwaka jana.

Hata hivyo, rekodi zinaonyesha kuwa JKT Tanzania huwa haina ubavu inapocheza dhidi ya Yanga. Kinachoweza kuibeba JKT Tanzania, labda ni kucheza kwenye uwanja mgeni kwa Yanga wa Jamhuri, tofauti na miaka yote ambapo imekuwa ikicheza mechi zote Uwanja wa Taifa au Uhuru jijini Dar es Salaam na si vinginevyo.

**JE, WAJUA?**



APRILI 2006, Alan Shearer alifunga bao lake la 260 na la mwisho kwake Ligi Kuu England [Premier League] ilikuwa wakati Newcastle ikishinda 4-1 dhidi ya Sunderland; hadi sasa ameendelea kuwa mfungaji bora wa wakati wote kwenye ligi hiyo.



# Stanbic Tanzania yaingia Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imefungua tawi jipya katika ya mkoa wa Dodoma ikiwa ni sehemu ya kuboresha utoaji huduma za kifedha kwa wateja wake.

Tawi hilo lililopo kati ya mtaa wa Mbeya na CDA mkoani humo, ni sehemu mkakati wa kupanua utoaji huduma ambao utasaidia wakulima, na kuimarisha biashara ndogondogo kupitia huduma za kifedha kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi, pamoja na mikopo nafuu.

Akizungumza juu ya uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Brian Ndadzungira, alisema: "Kumekuwa na ongezeko kubwa la watu na shughuli za kibiashara ndani ya mkoa wa Dodoma. Hivyo, uzinduzi wa tawi hili litawawezesha wateja wetu kupata huduma za kifedha zinazoweza kuchangia ukuaji wa shughuli za kiuchumi."

Pia aliongeza kuwa, benki hiyo ina mpango wa kuhakikisha inashughulikia changamoto na kutoa fursa kwa wateja wake hasa wafanyabiashara.

Huduma zitakazopatikana kwa ajili hiyo ni pamoja na huduma ya saa 24 ya Cash Deposit Machine ambayo itasaidia wafanyabiashara na watu binafsi kuweka pesa zao muda wote bila kikomo. Pia huduma zingine kama vile Vehicle Asset Finance (VAF) itarahisisha upatikanaji wa vifaa vya kilimo kwa ajili ya wakulima wa zao la zabibu na alizeti.

Hatua hiyo itachangia kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji na thamani ya bidhaa za viwanda kama vile mvinyo na mafuta ya kula. Mkoa wa Dodoma ndio unaoongoza katika uzalishaji wa zabibu nchini.

Aidha, alisema ufunguzi wa tawi hilo ni sehemu ya benki hiyo kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata huduma za kifedha ambazo zitaongeza uzalishaji na kuwatengenezea maisha bora.

"Tumedhamiria kuhakikisha kuwa huduma za kifedha tunazotoa ndani ya mji mkuu wa Dodoma zinakuwa na manufaa na matokeo endelevu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii," alisema Ndadzungira.

Hadi sasa benki ya Stanbic Tanzania imeifikia mikoa sita ambayo ni mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro na Dodoma.

**Hatua hiyo itachangia kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji na thamani ya bidhaa za viwanda kama vile mvinyo na mafuta ya kula. Mkoa wa Dodoma ndio unaoongoza katika uzalishaji wa zabibu nchini.**

# Makusanyo madini yavunja rekodi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imevunja rekodi ya makusanyo katika sekta ya madini, hadi kufikia Mei 31, mwaka huu imekusanya Sh. bilioni 479.45 malengo yaliyowekwa.

Hayo yalibainishwa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alipokuwa akizungumzia makusanyo hayo kupitia kipindi cha Dhukuru ya Msemaji kilichoandaliwa na Idara ya Habari (Maelezo).

Alisema katika mwaka wa fedha unaoisha wa 2019/20, serikali iliweka lengo la kukusanya Sh. bilioni 470 kupitia sekta hiyo, lakini hadi sasa zimekusanywa Sh. bilioni 479.45.

"Tunavyozungumza leo siku chache zilizopita tarehe 31 Mei 2020, Tanzania imevunja rekodi ya mapato katika sekta ya madini, utakumbuka miaka minne iliyopita tunaelekea mitano sasa," alisema.

Alieleza kuwa miaka iliyopita waliwahi kuweka lengo la kukusanya Sh.milioni 164 lakini walivunja rekodi na kufikia Sh. milioni 310.

"Kuna wakati tukavunja, tukaenda kwenye Sh. bilioni 310, tukavunja tukafika zaidi ya Sh. bilioni 400, mwaka huu wa fedha ambao tunaumaliza siku chache zijazo mwezi huu Juni tuliweka lengo gumu sana na wengi waliamini labda halitafikiwa la kukusanya mapato kwa mwaka yanayofikia Sh. bilioni 470," alisema.

Hata hivyo, alisema siku chache zilizopita hilo limevunjwa ikiwa ni mwezi mmoja kabla mwaka wa fedha kuisha rekodi imevunjwa, ambapo tayari Sh. bilioni 479.45 zimekusanywa.

"Hii ni serikali iliyopania kuleta mageuzi ya kweli kwa Watanzania na hii inatokana na msimamo binafsi wa Rais John Magufuli aliamini kuna kitu zaidi tunapaswa kukipata," alisema.

Aidha, alisema kitu kingine Rais Magufuli anaamini maono yake na anayasimamia.

"Ukiangalia hii miaka mitano, ametoa maelekezo mengi ikiwamo kuwapunguzia kodi wafanyabiashara wa sekta ya madini na wachimbaji wadogo, tukawahamasisha twende kwenye uwazi wachimbe madini na kupeleka kwenye masoko ambayo yameanzishwa mikoa yote tunakwenda sasa kwenye ngazi ya wilaya," alisema.

Aliongeza "Kingine alichokifanya ni kuzungusha ukuta wa Mererani watu wakazungumza sana wakalalamika kwamba kuzungusha ukuta sio suluhisho, leo yote haya ni matokeo ya jitihada za serikali chini ya Rais Magufuli."

Alisema Rais Magufuli anapoamua kufanya jambo lenye maslahi kwa Watanzania, mtu asikurupuke kupinga.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), akionyeshwa na Mkuu wa Kituo cha Michoro Miambani Kondoa, Zuberi Mabie, michoro ya miambani katika mapango ya Kondoa Irangi mkoani Dodoma, inayokadiriwa kuwa na zaidi ya miaka 10,000. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watafiti, vyuo vikuu watakiwa ushirikiano michoro mali kale

**Na Ibrahim Joseph, KONDOA**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, amewataka watafiti kushirikiana na vyuo vikuu ili kutafiti michoro ya mali kale na kuvumbua vivutio vingine iliyopo kwenye michoro hiyo.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki alipozungumza baada ya kutembelea eneo la michoro ya miamba kale iliyopo Kolo, Kondoa Irangi.

Alisema wakifanya utafiti zaidi kuhusu kuvumbua mabaki na vivutio vingine kwenye maeneo hayo itaongeza utalii.

"Natoa wito kwa watafiti wetu kushirikiana na vyuo vikuu kufanya utafiti wa mali kale zilizopo nchini na kuvumbua mabaki ya vitu vingine vilivyopo kwenye maeneo hayo," alisema.

Alisema baada ya kazi hiyo ya utafiti kukamilika wanatakiwa kuweka kwenye maandishi ili watalii wanapofika kwenye vivutio hivyo wajifunze historia nzuri ya maeneo husika.

"Mimi mwenyewe ni mara yangu ya kwanza kutembelea michoro hii ya Kondoa Irangi, nilikuwa naisikia na kuisoma nikiwa shule, lakini sasa nimejionea jinsi mababu zetu walivyoweza kutunza na kuhifadhi kumbukumbu hizi," alisema.

Alisema watu hao wa kale walijitahidi kutunza kumbukumbu kwa njia ya michoro ili kufikisha na kuhifadhi historia ya makabila na jamii husika.

Aidha, alisema dunia inarindima kutokana na watu weusi kudharaulika kwa kuwa hawakuendeleza utamaduni wa kuhifadhi historia ya kumbukumbu ya michoro ya kale iliyochorwa na mababu.

Alisema wazungu walipofika walifundisha utamaduni wa kuandika na kupoteza kumbukumbu ya utamaduni wa Waafrika uliojengeka wa kuweka kumbukumbu na ujumbe kwa njia ya michoro.

Alitoa wito kwa wananchi na familia zao kutembelea eneo la vivutio vya michoro hiyo kuona jinsi watu wa kale walivyokuwa wabunifu na uwezo mkubwa wa kuhifadhi vitu kwa njia ya michoro.

Naye, Mhifadhi Mkuu wa Mambo Kale wa Wizara hiyo, Revokatus Bugumba, alisema michoro hiyo ya mapango hayo ya Kondoa inashika nafasi ya pili katika maeneo ya vivutio michoro ya kale kusini mwa Afrika.

Bugumba alisema inayoongoza katika eneo hilo ni nchi ya Afrika ya Kusini, huku akitaja baadhi ya nchi zingine zilizo na uhifadhi huo wa michoro kale kuwa ni Nambia, Zimbambwe na Botswana.

Mkuu wa Kituo cha Michoro Miambani Kondoa Irangi, Zuberi Mabei, alisema michoro hiyo inakadiriwa kuwa na zaidi ya miaka 10,000 iliyopita.

Alisema michoro hiyo ya mapangoni inapatikana kwenye vijiji 13 vilivyopo kwenye eneo la hifadhi na mapango hayo yamekuwa yakitumika kufanya matambiko kwa makabila hayo mpaka leo.



# Jumuiya Wazazi yamwomba JPM kuingilia kati mfumo shule

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, imemwomba Mwenyekiti wa Chama hicho Taifa ambaye ni Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli kuingilia kati uendeshaji wa shule 14 za sekondari zinazomilikiwa na jumuiya hiyo, kutokana na kuwa na mfumo mbovu wa uendeshaji.

Wakizungumza juzi na waandishi wa habari, jumuiya hiyo ilisema shule hizo zinakabiliwa na matatizo mengi hasa ya kimfumo, hivyo wanamwomba Rais Magufuli pamoja na Katibu wa CCM, Dk. Bashiru Ally kuingilia kati suala hilo.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, James Mwampondele, alisema wamedhamiria kufikisha matatizo yanayozikabili shule hizo kwa Mwenyekiti wa Chama, Rais Dk. Magufuli ambaye ni mmiliki wa shule hizo.

"Tumepewa dhamana na Chama Cha Mapinduzi kusimamia shule hizo, kuna matatizo mengi ya kimfumo kwa muda mrefu, sasa tumekusudia kufikisha kilio chetu kwa Rais Magufuli ili atusaidie," alisema Mwampondele.

Alisema janga la corona limechangia kwa kiasi kikubwa kukosesha mapato kwa shule hiyo kwa madai kuwa shule zinategemea ada za wanafunzi kujiendesha.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Ivumwe, ambaye ni Mwenyekiti wa Shule zinazomilikiwa na jumuiya hiyo, Emmily Paul, alisema shule hizo zipo kwa ajili ya kutoa huduma na sio kutengeneza faida kwa sababu ada yake sio kubwa na zinalipwa kwa awamu nne na kwamba wanafanya hivyo ili kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini.

Alisema wakati shule zinafungwa mwezi Machi, wanafunzi walikuwa wamelipa ada ya miezi mitatu ambayo ni kuanzia Januari hadi Machi, kutokana na kufungwa shule, wameshindwa kupata mapato ya kuziendesha shule hizo ikiwamo mishahara ya wafanyakazi.

Miongoni mwa Shule zinazomilikiwa na jumuiya hiyo ni Shule ya Sekondari Meta, Sangu na Ivumwe ambazo miaka ya nyuma zilikuwa zikifanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa ukilinganisha na ilivyo sasa kutokana na matatizo mbalimbali kama vile ya kimfumo.




Meneja Mauzo wa Kanda ya Nyanda ya Kusini kutoka Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Abubakar Masoli (kulia), akimkabidhi moja ya mifuko yenye vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa corona, vilivyotolewa na kampuni kwa ajili ya kuwakinga wahudumu na wateja kwa Meneja wa baa ya Mwailubi iliyopo Mbeya, Danny Mwailubi (kushoto). Kampuni hiyo imetoa vifaa vya kinga na corona kwenye baa zaidi ya 2,500 nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali rufani yapewa cheti huduma bora watoto

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TAASISI inayotoa huduma kwa watoto wenye ulemavu wa mguu kifundo (TCCO) kwa kushirikiana na Shirika la Msaada kwa Watoto wenye nyayo zilizopinda Clubfoot - Miracle Feet, wamekabidhi cheti cha shukrani kwa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kutokana na jitihada wanazozifanya za kutoa huduma bora kwa watoto wenye tatizo la mguu kifundo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Akikabidhi cheti hicho mwishoni mwa wiki, Mratibu Msaidizi wa TCCO Nyanda za Juu Kusini, Ainael Sarinjo, alisema cheti hicho kina lengo la kutambua na kupongeza jitihada zinzofanywa na hospitali hiyo katika kuwahudumia watoto wenye tatizo la mguu kifundo licha ya uwepo wa janga la corona.

"Taasisi yetu imeridhishwa na huduma zinazotolewa na Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya katika kuwahudumia watoto wenye miguu kifundo, asilimia kubwa wanaohudumiwa hapo wanapona, tunaomba waendelee na moyo huo wa upendo kuwahudumia wanetu," alisema Sarinjo.

Akipokea cheti hicho kwa niaba ya viongozi na watumishi wa Hospitali ya MZRH, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Dk. Godlove Mbwanji alisema matibabu kwa watoto wenye mguu kifundo lazima yaendelee licha ya uwepo wa ugonjwa wa Covid-19.

Alisema hospitali hiyo inatoa huduma ya kliniki na matibabu ya mguu kifundo au nyayo zilizopinda ambao ni ulemavu unaotokana na matatizo ya mifupa na misuri ambayo ni wakuzaliwa nao na unaweza mpata mtoto yeyote duniani.

Aliwahamasisha wazazi na walezi wenye watoto ambao wanatatizo la mguu kifundo kutowaficha ndani badala yake wawapeleke Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya kupata matibabu kwa sababu wana kitengo maalum cha kuwahudumia watoto hao.

# Awataka kujihadhari na corona

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

MKUU wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amewahimiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Covid- 19 kwa kufuata ushauri wa kitaalamu ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa majisafi na sabuni.

Mfune aliyasema haya jana wakati akifungua warsha ya kujenga uwezo kwa jamii na kuimarisha mifumo ya serikali ili kupunguza kasi ya ongezeko la maambukizo ya Covid-19 na kuleta mabadiliko chanya dhidi ya mila, desturi na tabia zinazochangia maambukizo katika Mkoa wa Mbeya iliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Mbengonet.

Alisema kwa sasa wananchi wengi wamepuuza kuchukua tahadhari ikiwamo uvaaji wa barakoa maeneo yenye mikusanyiko hali ambayo inaweza kusababisha mlipuko wa ugonjwa huo ndani ya familia.


Alisema Shirika la Mbengonet liendelee kuisaidia serikali kutoa elimu dhidi ya kujikinga na corona kwa wananchi waishio vijijini ambako baadhi yao hawachukui tahadhari zozote.

"Tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya corona na tuache kuitafsiri vibaya kauli ya Rais Magufuli kuwa imeisha bali alisema imepungua kwa kiasi kikubwa, wako wanaopuuza taratibu za afya zilizowekwa ili kupunguza uwezekeno wa kuenea kwa ugonjwa huu hasa katika sehemu zenye mikusanyiko," alisema Mfune.

Naye Katibu Mtendaji wa Shirika la Mbengonet, Paul Kita, alisema kuwa wamejipanga kwenda kutoa elimu ya kujikinga na Covid- 19 na kuhamasisha matumizi ya barakoa na vitakasa mikono kwa waendesha bodaboda na bajaji pamoja na maeneo ya minada na magulio kwa kushirikiana na wataalamu wa afya kutoka serikalini.

Aliwakumbusha wananchi kuendelea kuzingatia usafi wa mwili na mazingira ili kuepukana na magonjwa mengine ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara.

**"Tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya corona na tuache kuitafsiri vibaya kauli ya Rais Magufuli kuwa imeisha bali alisema imepungua kwa kiasi kikubwa, wako wanaopuuza taratibu za afya zilizowekwa ili kupunguza uwezekeno wa kuenea kwa ugonjwa huu hasa katika sehemu zenye mikusanyiko," alisema Mfune.**





## Chadema kuweka mgombea urais wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwa mara ya kwanza tokea mfumo wa vyama vingi uanze, kinatarajia kusimamisha mgombea wa urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Chama hicho kwa Zanzibar hakijawahi kusimamisha mgombea urais licha ya kwamba uchaguzi wa mwaka 2015 kilikuwa ni miongoni mwa vyama vya siasa vilivyoungana na kuamua kumsimamisha mgombea urais, Maalim Seif Sharif Hamad kupitia CUF.

Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Salum Mwalimu, ametangaza nia ya kugombea nafasi hiyo ya urais wa Zanzibar, ambapo atachuana na vyama vingine vya siasa ikiwamo CCM.

Aliwataka wanachama wa chama hicho wenye sifa ambao wana nia ya kugombea nafasi hiyo, milango ipo wazi na kuanza mchakato wa kuomba nafasi hiyo ndani ya chama.

"Chama kimepima na kutafakari kwa kina na kimeona kwamba sasa ni wakati muwafaka kuwapa nafasi wanachama wake wenye ndoto na uwezo wa kugombea nafasi hiyo kutimiza ndoto zao," alisema.

Mwalimu alisema kuwa kufunguliwa kwa mlango huo wa kugombea urais wa Zanzibar, isiwe chanzo cha kuvuruga umoja na mshikamano ambao umekuwa thabiti ndani ya chama.

Alieleza kuwa pamoja na kufungua milango hiyo, chama hicho kipo tayari kuendeleza ushirikiano na vyama kulinda nia ya shabaha ya ushirikiano huo bila ya kuathiri malengo ya vyama vyao kwa maslahi ya Zanzibar katika uchaguzi mkuu.

"Hadi sasa nafasi ya urais haina mtu, hivyo kwa mwenye nia ya kutaka kugombea kujitokeze kuanzia leo Juni 6 hadi 15," alisema.

Aidha, alisema kwamba anaamini ushiriki wa chama chake katika kila hatua za uchaguzi mkuu zitakuwa za amani na bila ya kufanya vurugu ya aina yoyote.

"Kuanzia hatua hii ya kutangaza nia hadi katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu Chadema hatuta fanya vurugu ya aina yoyote ile, tutaendesha kwa amani na utulivu," alisema Salum Mwalimu.

Mwalimu alieleza kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita wamefanikiwa kuandaa mipango maalumu iliyoleta maboresho kupitia wadi, majimbo na mikoa kwa chama hicho.

Alieleza kwamba hadi sasa jumla ya watu 180 wameshajitokeza kugombe nafasi mbalimbali ya ubunge, udiwani na uwakilishi kupitia chama hicho.

Hata hivyo alisema chama hicho hakitegemei makundi wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu na kuwataka viongozi na wanachama kuwa kitu kimoja kwa jili ya ushindi.

Akizungumzia kuhusu daftari la wapigakura Zanzibar, alisema kuna baadhi ya wananchi wamekosa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na kushindwa kuwa na sifa ya kujiandikisha katika daftari la wapigakura, hivyo ni wajibu wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuliona hilo.

# ZEC kutorudia uhakiki wapigakura mara ya 3

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imesema haitarudia kwa mara ya tatu zoezi la uandikishaji na uhakiki wa daftari la wapigakura baada ya kumalizika kwa mara ya pili.

Akizungumza baada ya kutembelea vituo vya uandikishaji Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ofisa Uandikishaji Wilaya Kaskazini "A", Miza Pandu Ali, alisema uamuzi wa Tume wa kufanya uandikishaji kwa mara ya pili unatokana na juhudi zilizochukuliwa na Serikali ya Zanzibar na Tume hiyo kuhakikisha kila mwananchi aliyetimiza sifa za kuwamo katika daftari la kudumu la wapigakura anaandikishwa au kuhakikiwa taarifa zake.

Alisema kuwa zoezi hilo limerejewa tena kwa mara ya pili baada ya watu wengi kutopata fursa ya kujiandikisha katika daftari hilo baada ya kukosa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

"Hii ni awamu ya pili zoezi hili kurudiwa katika mikoa yote ya Unguja na Pemba, hivyo Tume haitegemei kurejea tena zoezi hili kwa mara ya tatu, ni vyema wananchi wakatumia fursa hiyo kujitokeza ili kuitumia haki yao hiyo," alisema.

Alieleza kuwa katika zoezi hilo la uandikishaji Tume hiyo inafuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona.

Kwa upande wao wananchi wa Wilaya hiyo ya Kaskazini Unguja wakiwa katika vituo vya uandikishaji waliipongeza Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa uamuzi waliouchukuwa kwa kufanya uandikishaji wa mara ya pili ikiwa na lengo la kutoa nafasi kwa wananchi ambao walikosa fursa hiyo katika zoezi la awali.

Katika hatua nyingine, ZEC iwataka makarani wa uandikishaji kuwa makini na kuzifuata sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi ili kutoa huduma bora wakati zoezi la uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura likiendelea katika vituo vya uandikishaji.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, alisema matarajio ya Tume ni kuandikisha idadi kubwa ya wananchi waliokosa fursa hiyo hapo awali, hivyo ni vyema makarani hao kuwa makini pale wanapotekeleza majukumu yao katika vituo vya uandikishaji.

Alisema ni matarajio ya Tume kuandikisha idadi kubwa ya wananchi ambao wamekosa fursa hiyo hapo awali, hivyo ni vyema makarani kuwa makini ili kuhakikisha kila mwananchi mwenye sifa ya kuandikishwa anakuwamo katika daftari la kudumu la wapigakura.

Alieleza kukamilika kwa kazi ya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura ni hatua muhimu ambayo itaiwezesha Tume kuweka wazi daftari, kugawa vitambulisho vya kupigia kura na kukamilisha kazi ya uchaguzi mkuu mwaka huu.



Mkazi wa Kijiji cha Kigunda Mkoa wa Kaskazini Unguja, Wanu Haji Kheri (kulia), akihakikiwa taarifa zake na mmoja ya wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi katika daftari la wapigakura katika kituo cha wapigakura cha Kigunda. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tamwa kusaidia kiuchumi waathirika kesi udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Zanzibar, kimesema kuwa katika kuhakikisha kesi za udhalilishaji zinatolewa ushahidi mahakamani, kimeamua kuwasaidia kiuchumi wazazi na walezi wa waathirika wa matukio hayo.

Hayo yalielezwa na Ofisa wa Sheria wa Tamwa Zanzibar, Ulfat Abdi, katika zoezi maalumu la utoaji wa vifaranga vya kuku kwa familia 15 za waathirika wa matukio hayo katika shehia tofauti za Unguja ili kujikomboa kiuchumi.

Alisema kwa kipindi kirefu kumekuwapo na baadhi ya wazazi na walezi kushindwa kufika mahakamani kutoa ushahidi wakati mwengine sababu kubwa ikitajwa kukosa nauli.

Alieleza kuwa Tamwa wameona ipo haja ya kuzisaidia familia hizo kuwapa vifaranga ambavyo anaamini wakivitunza vyema wataweza kuzalisha wengine na hatimaye kuwa chanzo cha kujingizia kipato.

Alisema jamii inapaswa kufahamu kuwa suala la kutoa ushahidi kwa kesi za udhalilishaji linapaswa kuzingatiwa na kuona umuhimu wake na kwamba bila ya ushahidi kesi hukosa nguvu na hatimaye mshtakiwa anaweza kuachiwa huru.

"Leo tunawapa vifaranga hivi ambayo kila kimoja kimegharimu shilingi 5,000, tukiamini kwamba utakuwa mwanzo mzuri kwenu wa kutunza kuku hawa na kuwa sehemu ya utatuzi wa changamoto zenu," alisema.

Waathirika wa udhalilishaji, walisema, si kama hawapendi kujitokeza mahakamani kutoa ushahidi, lakini wakati mwingine wamekuwa wakikosa nauli ya usafiri wa gari ya kuwafikisha huko, hivyo kesi zao hulazimika kuondoshwa mahakamani.

Mmoja wa mzazi ambae mtoto wake alibakwa (jina tunalihifadhi), alisema ni mara chache sana alizowahi kuhudhuria wito wa polisi kwa kukosa nauli, hivyo kusababisha kesi ya mtoto wake kusuasua.

Alisema kama si msaada wa majirani angeshindwa kuhudhuria kabisa kwenye kesi hiyo na anaamini isingeweza kwenda mahakamani.

Mkurugenzi wa Tamwa-Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliwatala wote walionufaika na mradi huo kuhakikisha vifaranga hivyo wanavitunza ili viweze kukua vizuri na kupata kipato.

Alisema anaamini kuku hao iwapo wahusika watawatunza vyema baada ya muda mchache wataweza kuzalisha wengine zaidi na kuwa chanzo kikubwa cha kujingizia kipato.

Zaidi ya vifaranga vya kuku 3,000 vimegaiwa kwa baadhi ya waathirika wa matukio ya udhalilishaji Unguja na Pemba kwa lengo la kujikomboa kiuchumi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ESSIO R. MPETTE** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina ya TOYOTA PROBOX yenye namba za usajili **T 193 CZN.** Chassis No. **NPC 50-0050274,** Engine **No.2NZ-3865604.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **NJ/TR//RB/477/2019.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 16 OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late FESTO DAUDI NGOWO Of Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for letters of administration by OMBENI NGOWO**

**GENERAL CITATION**

***(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)***

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 17 Day of 06, 2020.

Dated at Dodoma this 08 day of May, 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI Na.166 YA 2019**
**BAINA YA**
**LAURENT THOBIAS MASSAWE................................ MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**AKIBA COMERCIAL BANK PLC**
**BEST GROUP (T) LIMITED**
**EMANUEL SAMSON MSYANI.........................................WADAIWA**
**CRDB BANK PLC**
**MCHINGA AUCTION MART AND REAL AGENCY CO LTD**
**JAMES MOSES MARWA**

**KWA:-**
**BEST GROUP (T) LIMITED**
**EMANUEL SAMSON MSYANI CRDB BANK PLC**
**MCHINGA AUCTION MART AND REAL AGENCY CO LTD**
**JAMES MOSES MARWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI.**

Kwa kuwa Muombaji ameleta Maombi yake ambayo Maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili Kwa hiyo Mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa Kisheria tarehe 16.6.2020 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo Mnatakiwa kuleta utetezi wenu kwa Maandishi.
ANGALIZO:- kama hamkuhudhuria tarehe hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa mmepokea hati ya wito,Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yenu.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 ya mwezi wa Juni,2020.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 48/2020**

**Ombi la FATUMA HAMISI kuteuliwa**
**Msimamizi wa mirathi Marehemu HAMISI ABEID**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 01/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 05/6/2020.

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

---

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Nairobi, Mombasa zaendelea kufungwa

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ametangaza kuongeza marufuku ya kutotoka nje nchini humo, huku shughuli za usafiri katika Jimbo la Nairobi na Mombasa zikisitishwa kwa siku 30 zaidi.

Akizungumza katika Ikulu ya Nairobi, Rais Kenyatta aliondoa marufuku ya kutotoka nje katika maeneo ya Eastleig, na Old Town kuanzia saa 10 alfajiri. katazo lililotarajia kuanza jana.

Majimbo ya kwale na Kilifi pia yatafunguliwa kuanzia saa 10 asubuhi kwa sababu maambukizo yameanza kupungua katika maeneo hayo.

**Lazima tukubali kwamba siyo suala la kuwa uko sahihi au hauko sahihi, tumejikuta katika yote mawili ambayo ni sawa.**

Wakati huohuo, Rais Kenyatta amelegeza masharti ya kutotoka nje usiku, hatua ya kusalia ndani sasa itaanza kuanzia saa 3 usiku hadi saa 10 alfajiri.

Rais Kenyatta alifafanua kuwa kama kulegeza masharti kwa asilimia 20 kungesababisha maambukizo laki mbili na vifo 30,000 kufikia Desemba.

"Ikiwa masharti yangelegezwa kwa asilimia 60, kilele chake kingefikia Oktoba na maambukizo 450,000 na vifo 45,000," alisema Rais Kenyatta.

Rais Kenyatta alitolea mifano ya nchi zingine kama Korea Kusini, Pakistan na Malaysia na kuweka bayana kwamba ukosefu wa mchakato mahusus wa kufungua tena shughuli, maambukizo yanaweza kuongezeka zaidi au kupata wimbi la pili la maambukizo.

Alisema kituo kilichotengwa cha Siaya kina vitanda 10 na tayari watu 9 wamelazwa na kwamba kituo cha Busia kilichotengwa kuhudumia wagonjwa wa corona kina vitanda 34 na kituo hicho kilijaa wagonjwa siku mbili zilizopita.

Tangazo lingine ni shule kufunguliwa kuanzia Septemba mosi.

Baada ya kushauriana na washika dau wa elimu, Rais Kenyatta alisema Wizara ya Elimu pamoja na ya Afya, itatangaza mwongozo mpya na kuonyesha vile hali ya kawaida katika taasisi za masomo itakavyorejea taratibu kuanzia muhula wa tatu kuanzia Septemba mosi, 2020.

Wizara ya Elimu pia itatarajiwa kutangaza kalenda mpya ya shule katikati ya Agosti.

Rais Kenyatta alisema kuwa haikuwa kazi rahisi hata kwa timu yake ya wataalamu juu ya suala la kufunga au kufungua uchumi wa nchi.

"Lazima tukubali kwamba siyo suala la kuwa uko sahihi au hauko sahihi, tumejikuta katika yote mawili ambayo ni sawa. Wale wanaotaka kufungua uchumi wako sahihi na wale wanaopinga ufunguaji wa uchumi pia wako sahihi," alisema Rais Kenyatta.

Alisema kwamba hata yeye ni furaha na nia yake kufungua uchumi wakati huu kama ilivyo kwa raia.

Rais Kenyatta pia alitaka watu kuwa wa kweli na hali jinsi ilivyo na kusisitiza kwamba ikiwa hatua zilizopo zisinge. **BBC**




Wananchi wa Marekani wakiwa wameandamana mitaani kupinga vitendo vya ubaguzi wa rangi pamoja na manyanyaso ya Jeshi la Polisi. **PICHA: REUTERS**

## Mwandishi afariki kizuizini

**YAOUNDE,** Cameroon

JESHI la Polisi Cameroon limethibitisha kifo cha mwandishi wa habari, Samuel Wazizi, akiwa kizuizini.

Taarifa hiyo ya kifo cha mwandishi huyo zilitolewa na mashirika ya kiraia mwishoni mwa wiki, huku yakilaani vitendo vya kikatili alivyofanyiwa akiwa kizuizini, baada ya kushtumiwa na serikali kuwa anashirikiana na magaidi, kulingana na taarifa ya mashirika hayo.

Taarifa iliyotiliwa saini na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano katika Wizara ya Ulinzi imethibitisha kifo cha mwandishi huyo wa habari.

Kuhusu mazingira ya kifo chake, taarifa ya Wizara ya Ulinzi inabainisha kuwa baada ya kukamatwa Agosti 2 huko Ekona, Kusini-Magharibi mwa nchi, Samuel Wazizi ambaye jeshi linamtaja kama mweka hazina wa makundi mbalimbali ya kigaidi alikuwa amepelekwa kuhojiwa na idara husika mjini Yaoundé.

Hata hivyo alipokelewa kwenye idara hiyo akiwa katika hali mbaya ya kiafya na hivyo kupelekwa hospitalini mara moja. Lakini alifariki dunia siku chache baadaye, Agosti 17, 2019, kutokana na kipigo.

Hata hivyo, taarifa kutoka kitengo cha mawasiliano katika Wizara ya Ulinzi ilieleza kuwa hakufanyiwa kitendo chochote kile cha kikatili au mateso ya aina yoyote.

Kiongozi wa Chama cha Waandishi wa Habari nchini Cameroon (SNJC), Denis Nkwebo, alisema maelezo hayo ya Wizara ya Ulinzi ni ya kejeli kwa familia ya Samuel Wazizi na waandishi wa habari nchi Cameroon kwa ujumla. **RFI**

# Maandamano kupinga ubaguzi wa rangi yashamiri

**WASHINGTON,** Marekani

MAELFU ya waandamaji wameshiriki maandamano nchini Marekani na maeneo mengine duniani dhidi ya ukatili wa polisi na ubaguzi wa rangi.

Makamu wa Rais wa zamani wa Marekani, Joe Biden, alitumia mwanya huo kujipigia chapuo kisiasa kwa kutetea mabadiliko ya muundo wa Jeshi la Polisi kwa kile alichokiita hatua muafaka ya muda mrefu, sera kamili ya kubadili ubaguzi wa kimfumo. Endapo atachaguliwa katika uchaguzi wa Novemba.

Kupitia gazeti la kila siku la mjini Los Angeles, Los Angeles Times, Biden alisema endapo atachaguliwa atatunda kamisheni ya polisi ya taifa itakayoshughulikia masuala hayo ndani ya siku 100 akiwa ofisini.

Wakati hayo yanaelezwa, maofisa wawili wa polisi katika Jiji la Buffalo, katika Jimbo la New York wameshtakiwa kwa kufanya shambulizi, baada ya kuonekana katika video wakimsukuma mwandamanaji mzee wa umri wa miaka 75.

Katika video hiyo, mzee huyo alionekana akianguka chini, kichwa chake kujigonga katika lami, akapoteza fahamu na kuanza kuvuja damu.

Katika mji wa kaskazini/magharibi wa Marekani wa Seattle, kumeshuhudiwa maandamano ya siku ya tisa mfululizo, kufuatia kifo cha George Floyd.

Kundi kubwa la wafanyakazi wa sekta ya afya, na wengi wao wakiwa wamevaa mavazi ya maabara wameshiriki maandamano hayo.

Mwandamanaji mmoja alibeba bango lilioandikwa "Wauguzi wanapiga magoti nawe, sio kukupigia wewe." "Ukatili wa polisi na ubaguzi ni dharura ya afya ya umma."


Waandamanaji pia walijitokeza mjini New York, licha ya kuwapo kwa marufuku ya mamlaka ya jiji hilo ya kutotoka nje nyakati za jioni.

Mikusanyiko imefanyika siku nzima na jioni katika maeneo ya Manhattan, Brooklyn na Bronx. Wanasiasa wa watetezi wa haki za kiraia walijitokeza kuipinga marufuku iliyowekwa wakisema itasababisha makabiliano makali kati ya polisi na raia. Ujerumani na Uingereza pia watu walijitokeza kuunga mkono maandamano hayo.

Kwa Ujerumani watu wamekusanyika katika miji ya Cologne, Münster na Nuremberg, lakini kumeonekana makundi makubwa katika maeneo ya miji midogo kama Flensburg.

Nchini Uingereza katika jiji la London, Korea Kusini, Seoul pamoja na miji mingine duniani. **DW**

# POGBA, RASHFORD WAANZA MAZOEZI




**MANCHESTER,** England

WACHEZAJI wa Manchester United, Paul Pogba na Marcus Rashford wameanza mazoezi na kikosi hicho pale Old Trafford tangu Jumamosi.

Wawili hao walikuwa nje ya dimba kwa muda mrefu kabla ya ligi kusimama Machi mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Pogba ambaye aliumia kifundo cha mguu na Rashford mgongo, walirudi kwenye mazoezi kwa mara ya kwanza Jumamosi.

Nyota wa Ufaransa, Pobga yeye alikuwa nje ya dimba tangu Desemba 26, mwaka jana huku Rashford kwa mara ya mwisho aliichezea timu hiyo Januari 15.

Kurudi kwa wachezaji hao kutaongeza nguvu kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Ole Gunnar Solskjaer ambaye sasa atakuwa na matumaini ya kuwatumia katika mechi zilizobaki kumaliza msimu huu.

Kikosi hicho cha United kipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi kikipitwa pointi tatu na Chelsea waliopo nafasi ya nne na kitacheza na Tottenham kwenye mchezo wao wa kwanza wakati ligi ikirejea.

# Koeman: Ndoto yangu ni kuinoa Barcelona

**AMSTERDAM,** Uholanzi

RONALD Koeman amesema "kila mmoja anajua kwamba ndoto yangu ni kuwa kocha wa Barcelona", lakini Mdachi huyo bado ana majukumu na Uholanzi.

Koeman alihusishwa na Barca baada ya Ernesto Valverde kufukuzwa, kabla ya mabingwa hao wa LaLiga kumteua Quique Setien kuchukua mikoba yake Januari.

Beki huyo wa zamani wa Barca, Koeman awali alibainisha kwamba mkataba wake na Uholanzi una kipengele kilichoruhusu yeye kwenda Camp Nou baada ya Euro 2020, ingawa mashindano hayo yameahirishwa hadi mwakani kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Koeman, ambaye alifanyiwa upasuaji wa moyo Mei, ameelezea kuhusu uvumi wa kwenda Barca kwa siku za usoni.

"Nilipigiwa simu (kutoka Barca), kama nilivyokuwa ninaelezea mara nyingi. Lakini niliwaambia nimalize kwanza kazi na timu ya taifa, nilifikiria michuano ya Euro 2020 ingefanyika kipindi cha majira ya joto," alisema Koeman akiiambia Redio Catalunya.

"Nina furaha na namna mambo yanavyokwenda kwa timu ya taifa na mimi binafsi, hilo ni jambo muhimu sana kwa wakati huu. Hakuna kati yetu ajuaye nini kitatokea kwa siku za usoni."






# *Jadon Sancho ashauriwa kujitambua Dortmund*

**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho ameshauriwa na mchezaji mwenzake wa Borussia Dortmund, Emre Can "kukua" na kuimarika kwa nidhamu yake baada ya staili yake ya unyoaji wa mwenye kumuweka kwenye maji ya moto wiki hii.

Sancho alipigwa faini na Ligi Kuu ya Ujerumani, DFL, baada ya kuvunja sheria ya kujitenga kutokana na kuonekana akiwa nyumbani kwake na watu bila kuvaa barakoa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England aliita adhabu hiyo "hakika ni mzaha" kwenye Twitter yake kabla ya kuifuta.

Can, ambaye alifunga bao la ushindi dhidi ya Hertha Berlin Jumamosi, anataka kumuona mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 akionyesha kupevuka.

"Tunajua kwamba anatakiwa kuwa na nidhamu, lakini anajua mwenyewe," alisema Can akiiambia Sky.

"Anatakiwa kukua, kwani kuna vitu hatakiwi kuvifanya kama alivyofanya. Hatakiwi kufanya makosa ya mara kwa mara."

## HABARI MICHEZO

# DE LIGT ATOA MSIMAMO JUVENTUS




**TURIN,** Italia

MATTHIJS de Ligt amesisitiza kwamba uvumi wowote wa yeye kutaka kuondoka Juventus si wa kweli wakati akielezea furaha yake ya kuwa hapo Turin.

Mlinzi huyo wa kimataifa wa Uholanzi alitua kwa Bianconeri Julai mwaka jana kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 75 baada ya kuiongoza Ajax kushinda taji la Ligi Kuu na kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19.

De Ligt hivi karibuni aliripotiwa kwamba anaweza kuondoka hapo Juve, huku klabu ya Barcelona ikitajwa kuwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

Licha ya uvumi huo, De Ligt amebainisha kwamba hana mpango wa kuondoka katika timu hiyo kwa sasa.

"Kuna vitu vingi vinazungumzwa, lakini ukweli ni kwamba nina furaha sana kuwa hapa Turin na nikutana na wachezaji wengi wakubwa," alisema De Ligt akiliambia gazeti la Tuttosport.

"Nina hisia ya kuimarika kila siku. Ndio nina furaha kubwa kuendelea kucheza hapa.

"Wakati nilipotua Juve haraka nikajua kwamba hii ni klabu yenye malengo makubwa na hivyo nimeamua kujikita hapa."

# Klopp: Hatufikirii usajili kwa sasa

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema ni "bora kukaa kimya" kwa Liverpool katika suala la usajili, wakati akiwataja Timo Werner na Kai Havertz kuwa ni "wachezaji wa kiwango cha juu."

Liverpool imekuwa ikihusishwa sana na mshambuliaji wa RB Leipzig, Werner na kiungo mshambuliaji wa Bayer Leverkusen, Havertz katika miezi ya hivi karibuni.

Lakini ripoti zinabainisha kwamba watawakosa nyota hao wawili, huku Werner akikaribia kujiunga na Chelsea na Havertz akiwa kwenye rada za Bayern Munich.

Kocha wa Liverpool, Klopp ana furaha kutambua ubora wa wachezaji hao wakati akizungumza na Sky Sport Germany.

Lakini akaelezea kuwa mlipuko wa virusi vya corona unawafanya vinara hao wa Ligi Kuu ya England kutulia kwanza kabla ya kufanya kitu kikubwa kwenye usajili.

"Kuna wachezaji wengi wazuri katika sayari hii," alisema Klopp. "Timo Werner ni mchezaji mkubwa, Kai Havertz ni mchezaji mkubwa pia.

"Kwa sasa, nafasi na kila kitu kimekuja pamoja. Wiki sita au saba zilizopita hakuna aliyejua kama tutacheza mwaka huu.

"Na kwa sasa hatufikirii sana kuhusu usajili wa wachezaji wapya, tumetua kwanza na naamini baada ya muda fulani mambo yote yatakuwa sawa."







# *Mashabiki Benfica washambulia wachezaji*

**LISBON,** Ureno

WACHEZAJI wawili wa klabu ya Benfica wamepata majeraha na kukimbiziwa hospitali baada ya basi la timu hiyo kushambuliwa kwa mawe na mashabiki wenye hasira.

Hasira za mashabiki hao zilisababishwa na matokeo ya sare tasa ambayo timu hiyo ilipata dhidi ya Tondela katika mchezo wa Ligi Kuu ya Ureno.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema kwamba nyota hao walioku-tana na dhuruba hiyo ni kiungo Mjerumani, Julian Weigl na winga Mserbia Andrija Zivkovic ambao walilazimika kukimbiziwa hospitalini jijini Lisbon ili kupata matibabu kwa haraka.

Tukio hilo lilijiri muda mfupi baada ya mchezo huo ambao ni wa kwanza kwa Benfica tangu Ligi Kuu ya Ureno isimamishwe Machi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Licha ya kutokuwapo kwa mashabiki kwenye Uwanja wa Da Luz ambao unatumiwa na Benfica kwa michezo yake ya nyumbani, gari hiyo ilishambuliwa na kikundi cha mashabiki ambacho kilikuwa nje ya uwanja huo, mara baada ya mchezo kumalizika.

Mashabiki hao walionekana kukasirishwa na matokeo hayo ambayo yamewafanya kuwa na pointi sawa na wapinzani wao katika mbio za ubingwa, FC Porto kila timu ikiwa na alama 60, huku zikiwa zimebaki raundi tisa kabla ya ligi hiyo msimu huu kumalizika.

Uongozi Benfica umelaani kitendo hicho na kuahidi kushirikiana na mamlaka za ulinzi na za kisheria nchini humo kuwachukulia hatua wote walioshiriki vitendo hivyo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CORONA YAMWAHISHA SUAREZ BARCELONA

## ●●● Tayari mshambuliaji amethibitishwa na madaktari kuwa fiti kucheza...

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez amethibitishwa kuwa fiti kuichezea Barcelona katika mechi zao 11 zilizobaki kumaliza msimu huu 2019-20 baada ya kupona majeraha ya operesheni ya goti aliyofanyiwa Januari, mwaka huu.

**Suarez alifanyiwa upasuaji huo katika mguu wa kulia mwanzoni mwa mwaka, akiripotiwa kwamba alikuwa akisumbuliwa na maumivu kwa miezi kadhaa.**

Baada ya 'kupigwa kisu' hicho cha goti, Barca ilithibitisha kwamba atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi minne, na kuonekana kama angekuwa nje ya dimba kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki.

Lakini kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vilivyosababisha ligi kusimama na ikitarajiwa kuanza wiki ijayo, Suarez atakuwa tayari kuisaidia timu yake katika wiki zinazokuja, akiwa amerudi kwenye mazoezi kama mwezi mmoja uliopita.

Taarifa ya Barca iliyotolewa Jumamosi ilisomeka: "Luis Suarez tayari ameruhusiwa na yupo fiti. Siku 147 baada ya kufanyiwa upasuaji, mshambuliaji wa kimataifa wa Uruguay sasa amethibitishwa na madaktari wetu kuwa fiti na atakuwa sehemu ya kikosi cha kocha Quique Setien wakati ligi itakaporejea tena Juni 13."

Baada ya kuumia kwa Suarez na Ousmane Dembele, Barca walipewa ruhusu ya kufanya usajili wa mchezaji mmoja, Martin Braithwaite kutoka Leganes nje ya dirisha la usajili Februari, mwaka huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alicheza mechi tatu kwenye LaLiga kabla ya msimu kusimama, ingawa sasa atakuwa na wakati mgumu kugombea namba na Suarez.

Suarez mwenye umri wa miaka 33, alicheza wakati wakikumbana na kichapo cha 3-2 kwenye Supercopa de Espana dhidi ya Atletico Madrid, ambapo ulikuwa mchezo wa mwisho kwa kocha, Ernesto Valverde.

Setien alichukua nafasi ya Valverde Januari 13, siku moja baada ya Suarez kufanyiwa upasuaji.

Barca itarudi tena msimu huu wa 2019-20 ikiwa kileleni mwa msimamo ikiongoza kwa pointi mbili dhidi ya Real Madrid.

## ZISIKUPITE

### MADRID WAMFUATA KAI

REAL Madrid wametoa ofa ya euro milioni 80 kwa Bayer Leverkusen ili kumsajili Kai Havertz na watamruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 raia wa Ujerumani, kubakia katika klabu yake hiyo msimu ujao kabla ya kuhamia pale Bernabeu. ***(ESPN via Bild)***

### CHELSEA KUUZA NYOTA

CHELSEA itasikiliza ofa kwa wachezaji wake kadhaa baada ya kuripotiwa kumtarajia winga wa Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 27, kutoka Ajax na winga wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 24, kutoka RB Leipzig kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Daily Star on Sunday)***

### WERNER BADO CHELSEA

OFISA Mtendaji Mkuu wa Red Bull Leipzig, Oliver Mintzlaff amekanusha madai kwamba, Chelsea imefikia makubaliano ya kulipa pauni milioni 53 kwa ajili ya kumsajili Timo Werner. ***(Sky Sports Germany via Metro)***

### EVERTON YAMNYATIA RABIOT

KLABU ya Everton inaongoza kwenye mbio za kutaka kumsajili kiungo wa Juventus, Adrien Rabiot, 25, ambaye alipewa nafasi ya kucheza kwa mara ya kwanza katika timu yake ya zamani ya Paris St-Germain na kocha wa sasa wa Toffees hao, Carlo Ancelotti mwaka 2012. ***(Tuttosport via Mail on Sunday)***

### CHILWELL KAZI IPO CHELSEA

CHELSEA inakabiliwa na ushindani kutoka angalau klabu saba katika jaribio lao la kutaka kumsajili beki wa kushoto wa England, Ben Chilwell kutoka Leicester, ambao hawana presha ya kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Sunday Mirror)***

### ARSENAL YAMTAKA RUGANI

KLABU za Arsenal na Wolves zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa kimataifa wa Italia, Daniele Rugani mwenye umri wa miaka 25, ambaye hana namba katika kikosi cha kwanza cha Juventus chini ya Maurizio Sarri. ***(Tuttosport via Mail on Sunday)***

### KLOPP ASITA KWA WERNER

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amewaelezea Kai Havertz na Timo Werner kama wachezaji wakubwa, lakini hana uhakika wa kuwasajili. ***(Sky Sports)***

### MAN CIY YAIBIPU BARCA

KLABU ya Manchester City imewasiliana na Barcelona kuhusu mshambuliaji, Sergi Roberto. Lakini mchezaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 28, ataondoka Nou Camp ikiwa tu klabu hiyo itamwarifu kwamba sasa anaweza kuhamia kwingineko. ***(Mundo Deportivo)***

### LONGSTAFF KUTIMKIA WATFORD

KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Matty Longstaff mwenye umri wa miaka 20, huenda akaishia kwa wapinzani wao, Watford ikiwa atafikia makubaliano ya usajili kipindi hiki cha majira ya joto.

### INTER KUMUUZA SKRINIAR

KLABU ya Inter Milan inaweza kufikiria uwezekano wa kumuuza nyota wa Slovakia, Milan Skriniar, ambaye amehusishwa na Manchester City, ikiwa tu watapokea pendekezo la kumuuza mchezaji huyo kwa zaidi ya thamani ya euro milioni 80. ***(Tuttosport via Manchester Evening News)***

## Ligi Kuu Z'bar bila mashabiki Juni 20

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu ya Zanzibar inatarajiwa kuendelea kutimua vumbi Juni 20 katika kituo kimoja cha Kisiwani Unguja kwa timu zote 16 zinazocheza ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili Mkurugenzi wa mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohammed alisema ligi hiyo inatarajia kumalizika mapema Agosti 3, mwaka huu, huku shirikisho hilo likiendelea kujiandaa na msimu mpya.

Alisema ligi hiyo itachezwa kwa kuzingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Michezo pamoja na ile ya Afya Zanzibar katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Alisema kwa upande wa timu zilizopo Kituo cha Pemba zitawasili kisiwani Unguja pale Bodi ya Ligi na Kamati ya Mashindano zitakapotoa ratiba ya mchezo ya ligi hiyo.

Ligi Kuu Zanzibar inatarajiwa kurudi uwanjani bila ya mashabiki kwa hatua ya kwanza mpaka hapo serikali itakapotangaza vinginevyo.

## Kocha Prisons alia na washambuliaji

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Tanzania Prisons, Mohammed 'Adolf' Rishard, ameendelea kulia na safu yake ya ushambuliaji baada ya kueleza bado inampasua kichwa.

Akizungumza na Nipashe jana, kutoka mkoani Mbeya, Rishard alisema mpaka sasa timu yake haijawa na uwezo wa kugombania mpira, ikiwa ni pamoja na suala la umaliziaji kwa washambuliaji.

Kocha huyo alikiri kuona upungufu huo katika mchezo wa kirafiki walioucheza wiki iliyopita na dhidi ya Mbeya Kwanza inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Kocha huyo alisema tatizo hilo limedumu kwa muda mrefu ndani ya kikosi chake licha ya wachezaji kurejea wakitokea mapumziko ya corona wakiwa sawa, baada ya kufuata kwa makini maelekezo aliyokuwa amewapa.

# SVEN: WACHEZAJI SIMBA WANAREJESHA VIWANGO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema kwa sasa wachezaji wake wameanza kurejea kwenye viwango vyao vya kawaida, baada ya mazoezi ya siku 12 sasa.

**Kocha huyo alikuwa akizungumzia kiufundi juu ya maandalizi ya kikosi hicho kilichoanza kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na Kombe la FA kuanzia Mei 27, mwaka huu.**

Sven baada ya michezo kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na kuibuka mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona, alianza kukinoa tena kikosi hicho Mei 27, baada ya serikali kuruhusu tena michezo kuendelea nchini.

Alisema pamoja na kuwapa maagizo ya kufanya mazoezi nyumbani, lakini hawakuwa fiti kwa asilimia zote, hivyo kitu cha kwanza alichoanza nacho ni kuwarejeshea utimamu wa mwili.

"Tulikuwa na siku nne za kurudisha utimamu wao wa mwili ili wawe fiti, halafu baada ya hapo tukaja na siku kadhaa za kuwarejeshea uwezo wa kupambana mmoja mmoja na baada ya hapo siku hizi zilizobaki, tunachofanya ni kuwafundisha wachezaji mbinu za kimpira," alisema kocha huyo.

Jumapili ijayo kocha huyo atakuwa kwenye kibarua cha kwanza baada ya corona, Simba itakapopambana dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Sven ana mechi tano ya kuiwezesha Simba kutwaa ubingwa mara tatu mfululizo na kuingia kwenye vitabu vya kumbukumbu ya makocha walioiwezesha timu hiyo kongwe kufanya hivyo.

Kama Simba itatwaa ubingwa ambao utakuwa ni mara ya tatu mfulululizo, yeye mwenyewe itakuwa ni mara ya kwanza kuiwezesha timu hiyo kuchukua ubingwa, kwani msimu wa 2017/18 ilipotwaa ilikuwa chini ya kocha Mfaransa Pierre Lechantre, msimu wa 2018/19, ilitwaa chini ya Mbelgiji Patrick Aussems.

Sven anaweza kuwapiku makocha hao kama Simba itatwaa pia Kombe la FA, kwani chini ya makocha hao, timu hiyo iliondolewa mapema kwenye michuano hiyo.



Mshambuliaji Muivory Coast wa Azam FC, Richard Ella Djodi, akimtoka beki wa Transit Camp katika mchezo wa kirafiki uliopigwa usiku wa kuamkia jana katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam na kumalizika kwa sare tasa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Michezo mubashara sasa yarejea rasmi DStv

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa DStv wanauanza mwezi huu wa Juni kwa habari njema za kurejea kwa michezo mbalimbali kote ulimwenguni iliyokuwa imesitishwa kwa miezi kadhaa kutokana na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Na kuelekea kurejea kwa michezo hiyo, Kampuni ya MultiChoice Tanzania imethibitisha rasmi kuwa wateja wake wa kisimbuzi cha DStv wataanza kushuhudia michezo mubashara kuanzia katikati ya mwezi huu, ambapo michezo mingi iliyositishwa ikiwamo ligi kubwa na maarufu duniani kama ile ya Uingereza (Premier League), ya Italia (Serie A) na Hispania (La Liga) zinarejea na hivyo kuonyeshwa mubashara kupitia SuperSport kama ilivyokuwa hapo awali.

Akitangaza rasmi kurejea kwa michezo hiyo ndani ya DStv, Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, amewataka wateja wa DStv 'kukaa mkao wa kula' kwani burudani waliyoikosa kwa miezi michache sasa inarejea.

"Tunafurahi kuona kuwa michezo inafunguliwa sehemu mbalimbali duniani, na sisi kama vinara wa kuonyesha michezo hiyo, tayari tumejipanga kikamilifu kuwaletea wateja wetu burudani kabambe kupitia runinga zao," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na MultiChoice Tanzania, kwa upande wa kandanda, mashabiki wana kila sababu ya kusherehekea kwani ligi kubwa na maarufu barani Ulaya na duniani kote zinarejea.

Premier League, La Liga na Serie A zote zimethibitisha kurejea mwezi huu, ambapo La Liga itaanza kutimua vumbi ndani ya SuperSport jioni ya Alhamisi Juni 11 wakati watani wa jadi, Sevilla na Real Betis watakapoumana vikali. Kurejea kwa La Liga kutashuhudiwa mchuano wa aina yake kati ya Barcelona na Real Madrid wanaoongoza ligi hiyo kwa tofauti ya pointi mbili tu wakiendeleza mbio hizo.

Shughuli pevu itakuwa nchini Uingereza kwenye Premier League, itakayonguruma kuanzia Juni 17, mwaka huu kwa kuliwa viporo viwili – Manchester City watakapoumana na Arsenal, huku Aston Villa ya Mbwana Samatta wakivimbia ubavu na Sheffield United.

Macho na masikio ya mashabiki wa soka duniani yataelekezwa kwa vinara wa ligi hiyo - Liverpool ambao wanahitaji ushindi katika mechi mbili tu watangazwe mabingwa wa msimu huu. Kibarua chao cha kwanza kikiwa dhidi ya Everton mechi inayotarajiwa kuwa kali na ya kusisimua kwani bila shaka yoyote Everton hawatakubali kirahisi kuwa daraja la Liverpool kuelekea kwenye ubingwa.

Serie A nayo haijaachwa nyuma ambapo Juni 19-21 kutakuwa na 'patashika nguo kuchanika' wakati vinara wa soka nchini humo, Juventus watakapopigana vikumbo kuliwania kombe hilo.

Ikumbukwe bingwa mtetezi, Juventus ana pointi moja tu mbele ya Lazio ambayo msimu huu imeonekana kuwa timu matata sana kwenye ligi hiyo ya Italia. Internazionale nayo si ya 'kuchukuliwa poa' kwani inaweza kupindua meza ikiwa itafanya vizuri katika michezo yake iliyosalia.

Kwa wateja wa DStv, Woiso amesema kinachorejea siyo kandanda tu, bali michezo mingine kedekede hivyo watazamaji wa SuperSport wajiandae kwa burudani isiyo kifani. Michezo mingine maarufu kama Rugby, Golf, Riadha, UFC na mieleka - WWE yote inarejea kwa kishindo kikubwa.

# Michezo

Jumatatu Juni 8, 2020
Nipashe




Corona yamwahisha Suarez Barca UKURASA 22

BILA BARAKOA!...



Mashabiki wa Yanga na KMC FC, wakishuhudia mechi ya kirafiki wakati timu zao zikicheza katika Uwanja wa Uhuru jana, huku wengi wao wakiwa hawajachukua tahadhari ya maambukizo ya virusi vya corona kama ambavyo Wizara ya Afya inaagiza kuvaa barakoa hususan kwenye mikusanyiko kama hiyo. Katika mechi hiyo, KMC ilishinda 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Chama akamilisha chama la Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA la Wanamsimbazi sasa ni kama limekamilika baada ya kiungo wao mnyumbulifu, Mzambia Clatous Chama kuwasili nchini jana akitokea kwao Zambia tayari kujiunga na kikosi cha mabingwa hao watetezi wanaojiandaa na mechi za Ligi Kuu Bara pamoja na Kombe la FA.

Kutua kwa Chama inamaana Simba sasa inamkosa mchezaji mmoja tu, kiungo Msudan Sharaf Eldin Shaiboub, ambaye haijulikani ni lini atarejea nchini kutokana kutopata kibali cha kutoka kwao Sudan kwa sababu ya nchi hiyo kuendelea kuwa katika karantini ya janga la corona. Chama alitua jana mchana katika Uwanja wa Ndege wa JK Nyerere na kupokelewa na Mratibu wa timu hiyo, Abbas Ali, na anatarajiwa leo kuanza mazoezi na wenzake katika Uwanja wao wa Mo Simba Arena.

Taarifa kuutoka Simba zilieleza jana: "Kutoka Zambia hadi Tanzania kuja kuwatumikia Wanasimba na kuhakikisha wanapata burudani wanayostahili, Clatous Chota Chama amewasili nchini."

Hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Chama alishatupia mabao mawili na kutoa pasi za mwisho saba kati ya mabao 63 Simba iliyofunga.

Simba itarejea dimba Jumapili katika Uwanja wa Taifa kuikaribisha Ruvu Shooting kwenye mechi yao ya kiporo ya ligi hiyo wakati huu ikianza kusaka mechi tano za ushindi ili kutangazwa mabingwa wa ligi hiyo kwa mara ya tatu mfululizo.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Simba ndiyo iliyopo kileleni ikiwa na pointi 71, ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 54, hivyo Wekundu wa Msimbazi hao wanahitaji pointi 14 tu katika mechi zake 10 zilizosalia ili kufikisha alama 85 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote Ligi Kuu Bara.

# EYMAEL APAMBANA YANGA IKIFURUSHWA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

### ●●● Ni wakati ikilala 3-0 dhidi ya KMC, asema mambo magumu kuchomoka Ubelgiji, aahidi...

WAKATI kikosi chake kikikubali kipigo katika mechi ya kirafiki dhidi ya KMC FC jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amesema licha ya mipaka ya kwao kuendelea kufungwa kutokana na janga la corona, anapambana kuhakikisha anatua nchini keshokutwa, Jumatano kuendelea na majukumu yake ya kuiongoza timu hiyo kwenye mechi za Ligi Kuu zilizosalia pamoja na Kombe la FA.

**Yanga ambayo itakuwa ya kwanza kushuka dimbani kwenye Ligi Kuu baada ya kutangazwa kurejea Juni 13 kutokana na kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kufuatia kuibuka kwa mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), jana ilikubali kipigo cha mabao 3-0 kwenye mechi hiyo ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Uhuru.**

Mechi hiyo ilikuwa maalum kwa ajili ya wachezaji wa pande zote kujipima uwezo kabla ya kurejea kwa Ligi Kuu, ambapo Yanga Jumamosi itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Mwandu FC katika Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga, huku KMC ikisubiri hadi Juni 20 kuikaribisha Ruvu Shooting katika dimba la Uhuru jijini Dar es Salaam.

Awali uongozi wa Yanga ulitangaza kuwa Eymael angewasili nchini jana na kuendelea na kazi yake ya kukinoa kikosi cha timu hiyo, lakini hilo lilishindikana na jana kocha huyo akaliambia Nipashe kuwa anapambana kuhakikisha anarejea kabla ya mechi yao dhidi ya Mwadui licha ya mipaka ya kwao kuendelea kufungwa.

Akizungumza na Nipashe jana kwa simu kutoka Ubelgiji, Eymael alisema alitamani kurudi nchini mapema ila changamoto imekuwa ni mipaka kuendelea kufungwa kutokana na karantini ya corona.

"Hadi sasa nimekwama hii inachangia na masharti ya serikali kuwa magumu mipaka bado haijafunguliwa, na baada ya siku 31 zilizotolewa kuanzia Mei 31 ndipo ndege inaweza kupatikana ya kutoka Ubelgiji kuja jijini Dar es Salaam," alisema huku akisisitiza kuendelea kupambana ili ifikapo Jumatano awe amewasili nchini.

Eymael aliwataka mashabiki wa Yanga kuendelea kuvuta subira kwa kuwa mipango yake ni kurejea mapema.

"Mipango yangu ni kuwahi mechi dhidi ya Mwadui ila kutokana na hali ya nchi, sijui kama itawezekana, nina imani na kocha Charles [Boniface] Mkwasa kuendelea na programu yetu vizuri," alisema.

Wakati huo huo Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli naye alisema kutokana na changamoto ya mipaka timu itaendelea kubaki chini ya Mkwasa kwa kipindi chote hadi hapo Eymael atakapowasili.

Jana ikiwa chini ya Mkwasa, Yanga ilianza kukubali kipigo hicho dhidi ya KMC katika kipindi cha kwanza kupitia kwa Sadala Lipangile aliyeziona nyavu dakika ya 31 baada ya kuonana vema na wachezaji wenzake kabla ya kumchungulia kipa Metacha Mnata.

Baada ya bao hilo, KMC FC iliendelea kuliandama lango la Yanga na katika dakika za majeruhi kipindi cha kwanza, Martin Ilamfya aliipatia timu yake bao la pili kutokana na kuuwahi mpira mrefu kwa wazidi mbio mabeki wa Yanga na kuukwamisha kimiani.

Hadi mapumziko KMC ilikuwa mbele kwa mabao hayo na kipindi cha pili ikarejea kwa kasi ile ile kabla ya dakika ya 64, Hassan Kabunda kuukwamisha nyavuni mpira wa faulo baada ya kuchezewa madhambi na Kelvin Yondani karibu na eneo la hatari.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042